Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ofisi ya Makamu wa Rais

# MKAKATI WA TAIFA WA USIMAMIZI WA TAKA

## 2025 – 2030



2025

# DIBAJI



Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na jitihada mbalimbali za utatuzi wa changamoto za udhibiti na usimamizi wa taka nchini. Hata hivyo, pamoja na jitihada za Serikali katika kusimamia na kudhibiti taka, Tanzania imeendelea kukabiliwa na changamoto ya usimamizi usioendelevu wa taka ambao unaathiri afya ya binadamu na mazingira. Aidha, ukuaji wa miji na uchumi vimechangia ongezeko la uzalishaji wa taka katika maeneo mbalimbali nchini hivyo kuilazimu Serikali kuandaa mkakati wa usimamizi wa taka.

Serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka wa miaka mitano (2025 – 2030) wenye lengo la kuimarisha mfumo wa usimamizi wa taka ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira na kulinda afya ya jamii. Mkakati huu umeandaliwa kwa kuzingatia miongozo ya kimataifa, kikanda na kitaifa inayolenga kutatua changamoto za udhibiti na usimamizi wa mazingira. Miongozo hiyo ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya 2030; Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira; Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya mwaka 2025; Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; na Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032).

Mkakati huu utawezesha utekelezaji wa dhana ya uchumi rejeshi ambapo taka zinazozalishwa zinaweza kutumika tena kama malighafi viwandani. Utekelezaji madhubuti wa Mkakati huu utasaidia katika kupunguza kiasi cha taka kinachopelekwa dampo na kudhibiti uharibifu wa mifumo ikolojia. Vilevile, Mkakati huu utakuza uelewa wa jamii, kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kama njia jumuishi ya usimamizi wa taka na kuongeza ajira. Aidha, katika kufanikisha azma hiyo, Serikali imedhamiria kujenga mifumo madhubuti na kutenga rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati huu. Sanjari na hilo, Mkakati huu unalenga kushirikisha wadau wote katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira na athari za kiafya. Hivyo, ninatoa wito kwa wadau wote kutekeleza Mkakati huu wa usimamizi endelevu wa taka utakaochangia kuongeza kipato, kukuza uchumi wa nchi na uhifadhi wa mazingira.

…………………………………….

*Mhandisi* Hamad M. Y. Masauni (Mb.)

**WAZIRI WA NCHI**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO NA MAZINGIRA**

# SHUKURANI



Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka (2025 – 2030) umebeba dira na matumaini mapya katika kulinda mazingira yetu kupitia usimamizi madhubuti wa taka. Mkakati huu umeainisha kwa kina fursa lukuki zinazopatikana katika sekta ya usimamizi wa taka, sambamba na mbinu bunifu za kukabiliana na changamoto za uchafuzi wa mazingira nchini.

Maandalizi ya Mkakati huu yamewezekana kutokakana na ushirikiano mkubwa kutoka kwa wadau na wataalamu mbalimbali kutoka Wizara, Idara na Taasisi za Serikali; Mamlaka za Serikali za Mitaa; vyuo vya elimu ya juu; taasisi binafsi pamoja na asasi za kiraia. Ninapenda kutoa shukurani za dhati kwa kila mmoja aliyechangia kwa mawazo, maarifa na ushauri uliowezesha kufanikisha maandalizi ya Mkakati huu muhimu.

Kwa namna ya pekee, ninaishukuru Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA) kwa msaada wake wa kifedha na kitaalamu ambao umechangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha uandaaji wa Mkakati huu.

Vilevile, ninatambua kwa heshima kubwa mchango wa Viongozi na Wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa usimamizi na uratibu wa karibu uliohakikisha Mkakati huu unaandaliwa kwa weledi na kwa wakati.

Kwa pamoja, tumeweka msingi imara wa mustakabali wa mazingira yetu.

……………………

*Mhandisi* Cyprian J. Luhemeja

**KATIBU MKUU**

# YALIYOMO

DIBAJI ...... ii

SHUKURANI ...... ii

ORODHA YA MAJEDWALI ...... viii

ORODHA YA VIELELEZO ...... viii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ...... 1

1.1 Usuli ...... 1

1.2 Malengo ya Kimkakati ...... 1

1.4 Mawanda ya Mkakati ...... 2

1.5 Misingi ya Kisheria ...... 2

1.6 Mbinu Zilizotumika Kuandaa Mkakati ...... 2

5.2 Mapitio ya Nyaraka ...... 2

5.2 Vikao vya Wadau ...... 2

5.2 Warsha ya Uthibitishaji ...... 2

SURA YA PILI: JIOGRAFIA YA NCHI ...... 3

2.1 Jiografia na Idadi ya watu ...... 3

2.1 Tabianchi ...... 4

2.3 Masuala ya Kijamii na Kiuchumi ...... 4

a) Idadi ya Watu ...... 4

b) Makazi ya Watu ...... 4

c) Sekta za Uchumi ...... 4

SURA YA TATU: MFUMO WA KISERA NA KISHERIA ...... 5

3.1 Mfumo wa Kisera na Kisheria ...... 5

3.2 Tathmini ya Jumla ya Kisera ...... 7

SURA YA NNE: HALI YA USIMAMIZI WA TAKA ...... 8

4.1 Usimamizi wa Taka Ngumu ........ 8
5.2 Kiasi cha Uzalishaji, Vyanzo Vikuu na Mgawanyo wa Uzalishaji wa Taka. ........ 8
5.2 Utenganishaji, Uhifadhi, Ukusanyaji na Usafirishaji ........ 9
5.2 Dhana ya Upunguzaji wa Uzalishaji wa Taka (Tumia Tena, Urejelezaji na Uzalishaji wa Mboji) ........ 10
5.2 Utupaji Salama wa Taka ........ 11
4.2 Usimamizi wa Majitaka ........ 11
5.2 Usimamizi wa Topekinyesi ........ 12
5.2 Usimamizi wa Maji ya Mvua ........ 12
4.2 Tathmini ya Uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Usimamizi wa Taka ........ 13
4.3 Ugharimiaji wa Shughuli za Usimamizi wa Taka ........ 13
4.4 Jinsia katika Usimamizi wa Taka ........ 14
4.5 Kukuza uelewa kwa umma, ushirikishwaji wa jamii na Sekta Binafsi ........ 14
4.6 Changamoto na Fursa ........ 14
5.2 Changamoto ........ 14
5.2 Fursa ........ 15
SURA YA TANO: MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI ........ 17
5.2 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI ........ 17
5.12.1 Kuimarisha Upunguzaji wa Taka Kupitia Dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza ........ 17
5.2 Kuimarisha utenganishaji wa taka ........ 17
5.2 Kuanzisha na kuimarisha vituo vya utengenishaji wa taka ........ 17
5.2 Kuanzisha na/au kuimarisha vituo vya uzalishaji wa mboji ........ 18
5.2 Kuanzisha kituo cha kuzalisha nishati kwa kutumia taka ........ 18
5.2 Kuanzisha au kuboresha vituo vya mwisho vya utupaji wa Taka ........ 18
5.17.1 Kuimarisha Usimamizi wa Taka ........ 18
5.2 Kuimarisha ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi wa taka ........ 18
5.18.1 Kuimarisha Usimamizi Endelevu wa Majitaka ........ 18
5.2 Usimamizi wa majitaka na takakinyesi ........ 18

5.2 Kukuza na kuweka mifumo madhubuti na endelevu ya teknolojia za kutibu majitaka na takakinyesi 19
5.2 Kuimarisha programu za matumizi ya majitaka ... 19
5.2 Kuimarisha mifumo midogo ya uchakataji majitaka (DEWATS) ... 19
5.3 Usimamizi wa Maji ya Mvua ... 19
5.2 Kukuza usimamizi wa maji ya mvua ... 19
5.2 Kuimarisha usafi wa miundombinu ya maji ya mvua ... 20
5.24.1 Kuimarisha uwezo wa kitaasisi na Mfumo wa usimamizi wa Taka ... 20
5.2 Kuimarisha mfumo wa ugharimiaji usimamizi wa taka ... 20
5.2 Kuimarisha utekelezaji wa nyenzo za usimamizi wa taka ... 20
5.2 Kurasimisha wakusanyaji taka ... 20
5.2 Kuimarisha utafiti na kusambaza teknolojia bunifu ... 20
5.2 Kukuza Uelewa wa Umma, Ushirikishwaji wa Jamii na Sekta Binafsi ... 20
Lengo la Kimkakati 1: Kuimarisha Upunguzaji wa Taka kupitia dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza ... 25
5.2 Kuanzisha na kuimarisha vituo vya utengenishaji wa taka ... 26
Kuanzisha au kuboresha vituo vya mwisho vya utupaji wa Taka ... 27
Lengo la Kimkakati 2: Kuimarisha Ushughulikiaji wa Taka ... 27
Lengo la Kimkakati 3: Kuimarisha usimamizi endelevu wa majitaka ... 28
5.2 Kukuza matumizi ya mifumo midogo ya uchakataji majitaka ... 29
5.2 Kuboresha mfumo wa ugharimiaji usimamizi wa taka ... 30
5.2 Kuimarisha utekelezaji wa nyenzo za usimamizi wa taka ... 30
5.2 Mahitaji na Upatikanaji wa Rasilimali Fedha ... 36
5.3 Utaratibu wa Utekelezaji ... 36
5.3.1 Mamlaka za Serikali za Mitaa ... 36
5.3.2 Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ... 36
5.3.3 Wizara yenye dhamana ya Mazingira ... 37
5.3.4 Wizara yenye dhamana ya Afya ... 37

5.3.5 Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ... 37

5.3.6 Wizara za Kisekta ... 37

5.3.7 Idara na Wakala wa Serikali ... 37

5.3.8 Asasi za Kiraia ... 37

5.3.9 Sekta Binafsi ... 38

5.3.10 Taasisi za Elimu na Utafiti ... 38

5.3.11 Wadau wa Maendeleo ... 38

5.3.12 Wanajamii ... 38

5.3.13 Vyombo vya Habari ... 38

SURA YA SITA: UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI TAARIFA ... 39

6.1 Mpango wa Ufuatiliaji, Mapitio na Tathmini ... 39

6.1.1 Umuhimu wa ufuatiliaji ... 39

6.1.2 Umuhimu wa tathmini ... 39

6.1.3 Tathmini ya Utekelezaji wa Mkakati ... 39

6.2 Mpango wa utoaji wa Taarifa za Usimamizi wa Taka ... 40

6.2.1 Mpango wa Utoaji Taarifa Ndani ... 40

6.2.2 Mpango wa Utoaji Taarifa Nje ... 41

6.3 Utaratibu wa Ufuatiliaji wa Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Taka ... 42

Kuanzisha au kuimarisha vituo vya mwisho vya utupaji taka ... 44

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Uzalishaji wa Taka Ngumu na Mgawanyo wake katika baadhi ya Majiji na Miji ........8
Jedwali 2: Majiji yaliyo na mtandao wa uondoshaji wa majitaka kwa mwaka 2022/2023 .11
Jedwali 3: Mkakati wa Utekelezaji ........25
Jedwali 4: Ratiba ya utekelezaji wa Mkakati........40
Jedwali 5: Mpango wa Ndani wa utoaji taarifa........41
Jedwali 6: Mpango wa utoaji taarifa nje ........41
Jedwali 7: Matokeo ya utekelezaji wa Mkakati ........43
Jedwali 8: Orodha ya wataalam walioandaa Mkakati........49

# ORODHA YA VIELELEZO

kielelezo 1: ramani ya tanzania inayoonesha mikoa na mipaka ya nchi ........3

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Usimamizi wa taka ni mojawapo ya changamoto inayohitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa wakiwamo wazalishaji wa taka, wataalamu wa mazingira, watunga sera na jamii. Kama ilivyo kwa nchi nyingine, Tanzania inakabiliwa na changamoto ya usimamizi wa taka kutokana na shughuli zisizozingatia utunzaji wa mazingira, ukuaji wa miji na ongezeko la watu. Aidha, maeneo ya miji yanakadiriwa kuwa na uzalishaji mkubwa wa taka ambapo kiasi kinachokusanywa na kupelekwa dampo ni kidogo na hivyo sehemu kubwa ya taka hizo huchomwa na kutupwa katika maeneo ya wazi na kuathiri mazingira na afya ya jamii.

Sekta ya usimamizi wa taka nchini inaratibiwa na sera, sheria na kanuni mbalimbali ikiwamo Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191; na Sheria ya Afya ya Jamii, Sura ya 281 ambazo zimeweka mifumo ya kisheria ya usimamizi wa taka na kuainisha majukumu ya wadau mbalimbali ikiwamo Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kuimarisha udhibiti na usimamizi wa taka.

Pamoja na kuwapo kwa mifumo ya kisheria, usimamizi wa taka nchini unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo miundombinu duni, uhaba wa vifaa vya kukusanyia taka, upungufu wa vituo vya uchakataji na urejelezaji wa taka, na utupaji taka usiosahihi. Changamoto nyingine zinazochangia kuathiri jitihada za udhibiti na usimamizi wa taka ni pamoja na uelewa mdogo wa jamii, ufinyu wa bajeti na upungufu wa wataalamu wa mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, kuna ushiriki mdogo wa wadau ikiwamo sekta binafsi katika kutumia fursa zinazotokana na sekta ya usimamizi wa taka kama vile uzalishaji wa nishati kwa kutumia taka.

Usimamizi endelevu wa taka unaweza kuchangia kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) ya Umoja wa Mataifa, hususan upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira (SDG6); kuwapo kwa miji na jamii endelevu (SDG11); kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (SDG13); matumizi endelevu ya ardhi (SDG15); na uzalishaji na matumizi endelevu ya rasilimali (SDG12). Kwa muktadha huo, Serikali imeandaa Mkakati huu ili kuimarisha usimamizi wa taka utakaochangia kupunguza taka zinazopelekwa dampo, kuongeza ajira na kulinda mazingira na afya kwa jamii.

## 1.2 Malengo ya Kimkakati

Lengo kuu la Mkakati huu ni kuimarisha usimamizi endelevu wa taka ili kulinda afya ya jamii, kuhifadhi mazingira, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuchangia maendeleo ya kiuchumi nchini.

Malengo ya Kimkakati ni:

i) Kuimarisha upunguzaji wa taka kupitia dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza;
ii) Kuimarisha usimamizi wa taka ngumu;
iii) Kuimarisha usimamizi wa majitaka;
iv) Kuimarisha uwezo wa kitaasisi na mfumo wa usimamizi wa taka; na
v) Kukuza uelewa wa umma, ushirikishwaji wa jamii na sekta binafsi.

## 1.4 Mawanda ya Mkakati

Mkakati huu unalenga kuimarisha usimamizi wa taka ngumu na majitaka Tanzania Bara, isipokuwa taka za mionzi, taka za kielektroniki, taka hatarishi zinazotokana na shughuli za viwanda, huduma za afya, kilimo na uchimbaji madini ambazo zinaratibiwa na mikakati mahususi. Mkakati huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2025 – 2030).

## 1.5 Misingi ya Kisheria

Mkakati huu unaongozwa na misingi ifuatayo:

i) Msingi wa maendeleo endelevu: Maendeleo yanayokidhi mahitaji ya sasa pasipo kuathiri rasilimali kwa ajili ya vizazi vijavyo;

ii) Msingi wa kuchukua hadhari: Kuchukua hatua za awali za kudhibiti uharibifu wa mazingira;

iii) Msingi wa mchafuzi kulipa: Kuweka wajibu wa mchafuzi wa mazingira kulipa gharama ya uchafuzi uliofanywa;

iv) Msingi wa ushirikishwaji: Wadau wote wanapaswa kushirikishwa katika uamuzi wa masuala yanayohusu usimamizi wa taka;

v) Msingi wa uzingatiaji wa mipango na program mbalimbali: Kuhakikisha kuwa usimamizi wa taka unazingatia mipango, program na mikakati ya wizara, idara, taasisi na mamlaka zingine za Serikali; na

vi) Wajibu wa mzalishaji kudhibiti taka zinazotokana na bidhaa anazozalisha: Msingi huu umeweka sharti la wazalishaji kusimamia taka kuanzia hatua za uzalishaji hadi ukomo wake.

## 1.6 Mbinu Zilizotumika Kuandaa Mkakati

Uandaaji wa mkakati huu ulihusisha mbinu mbalimbali ikiwamo mapitio ya nyaraka, vikao vya wadau na warsha ya uthibitishaji.

### 5.2 Mapitio ya Nyaraka

Hatua hii ilihusisha uchambuzi wa nyaraka mbalimbali ili kubaini hali na njia zinazotumika katika usimamizi wa taka nchini. Takwimu na taarifa kutoka vyanzo mbalimbali zilichambuliwa ili kubaini hali na mbinu zinazotumika katika usimamizi wa taka nchini.

### 5.2 Vikao vya Wadau

Hatua hii ilihusisha vikao tisa (9) vya wataalamu na wadau kuhusu usimamizi wa taka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, taasisi za serikali, sekta binafsi na asasi za kiraia.

### 5.2 Warsha ya Uthibitishaji

Hatua hii ilihusisha vikao viwili (2) vya mapitio na uhakiki wa takwimu zilizotumika ili kuboresha Mkakati huu. Mkakati uliwasilishwa kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kufanya mapitio, kutoa maoni na mapendekezo ya kuboresha mkakati huo kwa ajili ya uandaaji wa toleo la mwisho, uchapishaji na utekelezaji.

# SURA YA PILI: JIOGRAFIA YA NCHI

Sura hii inaeleza ukubwa wa eneo la nchi, idadi ya watu, hali ya hewa na masuala ya kijamii na kiuchumi.

### 2.1 Jiografia na Idadi ya watu

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipo katika ukanda wa Afrika Mashariki ikiwa na eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 948,740 kati ya longitudo 29° hadi 41° Mashariki na latitudo 1° hadi 12° Kusini. Upande wa Kaskazini inapakana na nchi za Kenya na Uganda, upande wa Magharibi inapakana na nchi za Rwanda, Burundi, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Upande wa Kusini-magharibi, inapakana na nchi za Zambia na Malawi, na Kusini inapakana na nchi ya Msumbiji. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Tanzania ilikuwa na idadi ya watu milioni 61.7.




**Kielelezo 1: Ramani ya Tanzania inayoonesha Mikoa na Mipaka ya Nchi**

## 2.1 Tabianchi

Hali ya hewa ya nchi ina pepo za aina mbili ambazo ni Pepo za Kaskazi na Pepo za Kusi. Pepo za Kusi huanza mwezi Aprili hadi Septemba. Pepo hizi zina kasi na mara nyingi hutokea upande wa Kusini mwa nchi. Aidha, pepo hizi zina kiwango cha chini cha joto cha takriban sentigredi 25 na huleta mvua za masika. Pepo za Kaskazi huanza mwezi Novemba hadi Februari. Pepo hizi ni nyepesi na mara nyingi hutokea upande wa kaskazini mwa nchi. Aidha, Pepo za Kaskazi huambatana na hewa yenye kiwango cha juu cha joto la zaidi ya sentigredi 30 ambalo huleta mvua za vuli kuanzia mwezi Novemba hadi Disemba. Wastani wa unyevu nchini unakadiriwa kuwa asilimia 44.6 ambapo kila mwezi hubadilika kwa kiwango cha kati ya asilimia 30 mwezi Septemba na Oktoba hadi 58 mwezi Machi. Maeneo ya ukanda wa pwani yana unyevu mwingi kuliko maeneo mengine ya nchi.

## 2.3 Masuala ya Kijamii na Kiuchumi

### a) Idadi ya Watu

Kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, idadi ya watu nchini ni milioni 61.7 na inakadiriwa kukua kwa asilimia 3.2 kwa mwaka. Aidha, inakadiriwa kuwa idadi ya watu itaongezeka mara mbili na kufikia milioni 89.2 ifikapo mwaka 2035 katika kipindi cha miaka 22 ijayo. Ukuaji huu wa idadi ya watu unaweza kuchangia kwenye uchafuzi wa mazingira kutokana na ongezeko la kiwango cha taka kinachozalishwa. Wakati uzalishaji wa taka ukiongezeka, bado hali ya ukusanyaji na utupaji wa taka ni changamoto ambapo takribani asilimia 40.5 ya kaya huchoma taka ikiwa ni moja ya mbinu ya kutupa taka ikifuatiwa na asilimia 21.4 ya kaya ambazo hutumia mfumo wa kawaida wa ukusanyaji wa taka huku asilimia 14.4 ya kaya huchimba mashimo na kufukia taka.

### b) Makazi ya Watu

Maendeleo ya makazi ya watu nchini yamekuwa si endelevu kutokana na uzingatiaji hafifu wa masuala ya kijamii na kiuchumi katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira, jambo ambalo limechangia uzalishaji wa taka katika maeneo mbalimbali ikwamo katika miji. Aidha, ongezeko la makazi yasiyozingatia mipango miji katika miji sambamba na uhaba wa miundombinu na huduma muhimu yamechangia udhibiti hafifu wa taka na kuwa tishio kwa mazingira na afya ya jamii.

### c) Sekta za Uchumi

Pato la Taifa kwa mwaka 2023 lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta za kilimo (mazao, mifugo, misitu na uvuvi) asilimia 26.5, miundombinu asilimia 13.2, biashara na huduma asilimia 8.3, uzalishaji viwandani asilimia 7.0, na madini asilimia 9.0.

# SURA YA TATU: MFUMO WA KISERA NA KISHERIA

Sura hii inabainisha Sera za kitaifa zilizopo na mfumo wa kisheria unaolenga kukuza usimamizi endelevu wa taka. Pia, inaeleza upungufu uliopo katika sera hizo, hususan katika utekelezaji wa dhana ya uchumi rejeshi, ambao unaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika usimamizi wa taka.

## 3.1 Mfumo wa Kisera na Kisheria

Usimamizi wa taka nchini unaongozwa na nyenzo mbalimbali ikiwamo Sera ya Taifa ya Mazingira (2021) inayoainisha miongozo ya kisera katika usimamizi wa taka nchini. Aidha, Serikali imeandaa mikakati, mipango, programu na miongozo mbalimbali ikiwamo: Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka (2022-2032); Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji), Sura ya 288; Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya), Sura ya 287; Sheria ya Afya ya Umma, Sura ya 281; na Sheria ya Mipango Mjini, Sura ya 355.

**Sera ya Taifa ya Mazingira (2021**)

Sera hii inalenga kutoa mwongozo wa kitaifa wa usimamizi wa mazingira ikiwamo udhibiti wa taka. Aidha, sera hii inahamasisha udhibiti na usimamizi endelevu wa taka, ushiriki wa sekta binafsi na utoaji wa elimu kwa umma.

**Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032)**

Mpango Kabambe unalenga kutoa mwongozo na hatua za kuchukuliwa katika kutatua changamoto za mazingira nchini kwa kuzingatia sehemu zinazohusika na hatua mahususi zinazotakiwa kuchukuliwa ikiwamo usimamizi wa taka. Pia, Mpango huu umeainisha hatua kadhaa zinazozingatia kupunguza uzalishaji wa taka, kutumia tena na kurejeleza taka kwa lengo la kufikia mfumo wa uchumi rejeshi.

**Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191**

Kifungu cha 114-138 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kimetoa jukumu la usimamizi wa taka ngumu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upunguzaji na utenganishaji wa taka unaofanyika katika vyanzo vya uzalishaji wa taka ngazi ya kaya. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepewa jukumu la kufanya tafiti za mara kwa mara za uzalishaji wa taka ili kutumia mbinu sahihi za uchambuaji, uhifadhi, usafirishaji na utupaji salama wa taka. Vilevile, zina jukumu la kusimamia ukusanyaji wa taka katika maeneo ya mijini na pembezoni mwa miji na kuanzisha mfumo wa usafirishaji na utupaji salama wa taka. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kusimamia na kuhakikisha viwanda vinasimamia ipasavyo taka zote zinazozalishwa kutokana na shughuli zao.

**Sheria ya Afya ya Jamii Sura ya 281**

Kifungu cha 73-76 cha Sheria ya Afya ya Jamii kinaelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha usafi wa mazingira na kudhibiti taka (taka ngumu na majitaka) ili kuzuia kuenea kwa magonjwa. Vilevile, Mamlaka za Serikali za Mitaa zina jukumu la kufanya tafiti za mara kwa mara kuhusu uzalishaji na utenganishaji wa taka ngumu.

**Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji), Sura ya 288 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya), Sura ya 287**

Kifungu cha 55 cha Sheria kinatoa jukumu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia miundombinu ya usimamizi wa taka katika eneo la kimamlaka, ikiwa ni pamoja na eneo maalumu la kutupa taka (dampo), vyoo vya umma, na vifaa vya kuhifadhia taka.

**Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Sura ya 272**

Kifungu cha 20 cha Sheria hii kinaelekeza Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira kusimamia vyanzo vya maji, viwango vya ubora wa maji na uhifadhi wa mazingira.

**Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355**

Sheria hii inaelekeza utaratibu na michakato ya mipango ya matumizi ya ardhi, uendelezaji miji na kusimamia utekelezaji wa mipango inayohusika. Sheria inaeleza kanuni za msingi za matumizi ya ardhi, kuanzisha taratibu za upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini. Sheria inainisha masuala yanayopaswa kuingizwa katika mipango yote ya matumizi ya ardhi ikiwamo inayohusiana na maji na rasilimali misitu. Pia, Sheria hii inaweka masharti ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira.

**Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa Taka ngumu) za Mwaka, 2009**

Kanuni hizi zinaelezea majukumu ya usimamizi wa taka ngumu nchini. Pia, Kanuni hizi zinasisitiza upunguzaji wa taka kwa kuzingatia misingi endelevu ili kulinda afya ya jamii na mazingira.

**Mwongozo wa Udhibiti wa Taka Ngumu kwa Kutumia Dhana ya Punguza,Tumia Tena na Rejeleza wa (2021)**

Mwongozo huu unaelekeza utekelezaji wa dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza katika usimamizi endelevu wa taka. Pia, Mwongozo huu umebainisha hatua mahususi zinazopaswa kutekelezwa na wadau mbalimbali katika kufanikisha malengo ya dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza.

**Sheria za Serikali za Mitaa**

Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zimeandaa sheria ndogo za usimamizi wa taka katika maeneo ya mamlaka husika. Hata hivyo, mapitio ya baadhi ya sheria ndogo yanaonesha upungufu katika mipango ya usimamizi wa taka katika halmashauri. Aidha, sheria hizo zimebainisha kutokuwapo kwa usimamizi jumuishi wa taka na hazitambui umuhimu wa wakusanyaji na wachambuzi wa taka ngumu, na zina upungufu katika mfumo wa ufuatiliaji, ukusanyaji, utenganishaji, uhifadhi, usafirishaji, uchakataji, urejelezaji na utupaji salama wa taka.

### 3.2 Tathmini ya Jumla ya Kisera

Tathmini ya sera zilizopo na mifumo ya kisheria ya usimamizi wa taka inaonesha upungufu katika utekelezaji wa uchumi rejeshi. Upungufu huo ni pamoja na:

i) Kutokuwapo kwa motisha ya utenganishaji wa taka katika vyanzo vya uzalishaji;
ii) Kutokuwa na mfumo wa kusimamia ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za usimamizi wa taka;
iii) Kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa utenganishaji wa taka katika vyanzo;
iv) Kutokuwa na mwongozo madhubuti wa ugharimiaji endelevu wa huduma za usimamizi za taka nchini;
v) Kutokuwa na mwongozo wa kisheria kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa na kutekeleza mipango ya usimamizi wa taka iliyolenga maeneo husika;
vi) Upungufu wa miundombinu ya usimamizi wa taka; na
vii) Kuwapo kwa Sheria ndogo za mazingira zilizopitwa na wakati.

Ili kukabiliana na upungufu huo, mbinu ya uchumi rejeshi inapendekezwa, ambayo inalenga kudumisha matumizi ya bidhaa, vifaa na miundombinu kwa muda mrefu zaidi, hivyo kuongeza tija ya rasilimali zitokanazo na taka.

# SURA YA NNE: HALI YA USIMAMIZI WA TAKA

Sura hii imebainisha hali ilivyo katika usimamizi wa taka nchini, hususan taka ngumu, majitaka na maji ya mvua. Aidha, imeainisha changamoto na fursa zilizopo katika usimamizi wa taka ngumu kupitia dhana ya uchumi rejeshi.

**4.1 Usimamizi wa Taka Ngumu**

**5.2 Kiasi cha Uzalishaji, Vyanzo Vikuu na Mgawanyo wa Uzalishaji wa Taka.**

Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, kwa sasa uzalishaji wa taka ngumu nchini unakadiriwa kuwa takriban tani milioni 14.4 - 20.7 kwa mwaka ikiwa ni sawa na kilogramu 0.66-0.95 za uzalishaji kwa kila mtu kwa siku. Hali hii inaonyesha kuwa kwa wastani, kila mtu huzalisha kati ya kilogramu 241 - 347 za taka ngumu kila mwaka. Vyanzo vikuu vya uzalishaji wa taka ngumu ni pamoja na kaya (75%), viwanda na maeneo ya biashara (20%), taasisi (0.5%), masoko (3.5%) na usafishaji wa barabara (0.5%).

Aidha, inakadiriwa kuwa kati ya asilimia 40-50 ya taka ngumu huzalishwa katika maeneo ya mijini. Hata hivyo, hakuna mfumo rasmi wa ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa taka ngumu nchini. Takwimu zilizopo zinatokana na taarifa chache zilizokusanywa kutoka katika miji mikubwa ikiwa ni pamoja na miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza, na Tanga. Hali hii ikimaanisha kuwa shughuli za usimamizi wa taka ngumu zinafanyika zaidi katika kata chache za miji mikuu, huku maeneo mengi ya mijini na pembezoni mwa miji yakikosa huduma za ukusanyaji wa taka.

Uzalishaji na mgawanyo wa uzalishaji wa taka ngumu hutofautiana kati ya miji nchini (Jedwali 1). Kulingana na takwimu kutoka kwenye baadhi ya majiji nchini, mgawanyo wa uzalishaji wa taka ngumu unahusisha takaozo hususan (taka za bustani, kuni na mabaki ya chakula) ambazo huchangia wastani wa asilimia 63.4, karatasi asilimia 6.1, plastiki asilimia 12, kioo asilimia 4.2, metali/chuma asilimia 1.5, na taka nyinginezo (kama vile nguo chakavu, ngozi, mpira, taka za kielektroniki na majivu) kwa asilimia 12.8.

**Jedwali 1: Uzalishaji wa Taka Ngumu na Mgawanyo wake katika baadhi ya Majiji na Miji**

| Jiji | Uzalishaji (Tani/siku) | Takaozo (%) | Karatasi (%) | Kioo (%) | Plastiki(%) | Chuma (%) | Nyinginezo(%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 338 | 56 | 9 | 4 | 18 | 2 | 11 |
| Dar es Salaam | 9000 | 44.5 | 12 | 9 | 22 | 0.5 | 12 |
| Mbeya | 380.57 | 79.58 | 3.01 | 2.34 | 5.36 | 3.24 | 6.47 |
| Moshi | 214.4 | 73.44 | 0.33 | 1.69 | 2.66 | 0.13 | 21.75 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 362 | 68 | 9 | 3 | 7 | 2 | 11 |
| Tanga | 217 | 17 | 9.10 | 4.31 | 11.23 | 9.49 | 3.91 |
| Mwanza | 357 | 60 | 5 | 5 | 10 | 0.2 | 19.8 |

**Chanzo:** Ofisi ya Makamu wa Rais (2024)

### 5.2 Utenganishaji, Uhifadhi, Ukusanyaji na Usafirishaji

Utenganishaji wa taka ngumu nchini unatekelezwa zaidi na sekta zisizo rasmi zinazojumuisha wakusanyaji wa taka na warejelezaji wadogo wa taka. Utenganishaji wa taka ngumu unafanywa zaidi katika kaya na maeneo ya biashara kwa lengo la kupata taka zinazoweza kutumika tena na/au kurejelezwa, taka hizo ni pamoja na karatasi, plastiki, vioo na chuma chakavu. Aidha, kiasi cha taka kinachoweza kurejelezwa hakiwezi kukadiriwa kwa urahisi kwa kuwa ukadiriaji wa kiasi cha taka zinazoweza kurejelezwa unategemea aina na ubora wa taka na masoko yaliyopo kwa wakati huo.

Vilevile, idadi ya wakusanya taka inatofautiana katika maeneo mbalimbali kulingana na upatikanaji wa taka na idadi ya viwanda vya urejelezaji wa taka vilivyopo katika eneo linalohusika. Katika kuhakikisha wakusanya taka wanatambuliwa na kurasimishwa, tayari wakusanya taka zaidi 2,000 wamesajiliwa katika miji mikubwa. Utenganishaji wa taka usioridhisha unasababishwa na masuala mabalimbali ikiwamo uelewa mdogo miongoni mwa jamii, ukosefu wa motisha na kutokuwapo kwa vituo vya utenganishaji wa taka. Hali hii inaweza kusababisha kuzagaa kwa taka ngumu kwenye mazingira na kuathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za urejelezaji wa taka ngumu.

Katika hatua za usimamizi wa taka, taka zinaweza kuhifadhiwa kwa muda kabla ya kupelekwa dampo hususan katika kaya, vituo vya kukusanyia taka ngumu, na maeneo ya biashara na viwandani. Aidha, maeneo ya biashara na viwanda huzalisha kiasi kikubwa cha taka ngumu hivyo kuhitaji mkakati maalum wa kuhifadhi taka. Vifaa vya kuhifadhia taka hizo ni pamoja na makasha au mapipa ya kuhifadhia taka, au maeneo maalumu ya kuhifadhi taka kulingana na Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Ngumu za Mwaka 2009.

Aidha, ni takribani asilimia thelathini na tatu (33%) tu ya taka ngumu zinazozalishwa hukusanywa nchini kote. Vilevile, halmashauri za majiji zinazalisha kwa wingi taka ngumu ikilinganishwa na halmashauri za miji. Aidha, takwimu za ukusanyaji wa taka ngumu kutoka halmashauri za manispaa zinaonyesha ufanisi wa ukusanyaji unaozidi asilimia hamsini (50%), ikiwa ni pamoja na Mwanza asilimia tisini na tano (95%), Arusha asilimia sabini na moja (71%), Tanga asilimia sitini na tatu (63%) na Dodoma asilimia hamsini na tatu (53%). Wahusika wakuu wa ukusanyaji na usafirishaji wa taka kwenda dampo ni pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, vikundi vya kijamii, kampuni binafsi na vikundi vya ukusanyaji wa taka.

Vifaa vinavyotumika katika usimamizi wa taka ni pamoja na malori ya kukusanya na kusafirisha taka nchini; makasha ya kuhifadhia taka; malori yenye mashine za kusaga na kubeba taka; magari ya

kusafisha barabara; mitambo ya kushindilia (kompakta), kupakia na kupakua taka; na magari ya ukaguzi na usimamizi wa taka.

Aidha, vikundi vya kijamii (vijana na wanawake) vimekuwa vikishirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika shughuli za usimamizi wa taka ngumu. Jitihada hizi zimekuwa zikichangia ongezeko la ajira japokuwa zinakabiliwa na changamoto kubwa ikiwamo uchakavu wa miundombinu (vituo vya ukusanyaji wa taka, vituo vya urejelezaji wa taka); ukosefu wa uhakika wa masoko; kutokuwapo kwa mpango rasmi wa mafunzo kwa wadau; na ukosefu wa raslimali fedha kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa taka.

Changamoto katika ukusanyaji na usafirishaji wa taka ngumu ni pamoja na gharama kubwa za uendeshaji zinazochochewa na umbali mrefu wa usafirishaji wa taka; kutoweza kufikiwa kwa baadhi ya maeneo yanayozalisha taka ngumu; uchakavu wa magari ya kukusanya taka; kutolipa wakandarasi kwa wakati; uelewa mdogo wa jamii katika usimamizi wa taka; na ukosefu wa mifumo ya dijitali wa kanzidata ya usimamizi wa taka.

## 5.2 Dhana ya Upunguzaji wa Uzalishaji wa Taka (Tumia Tena, Urejelezaji na Uzalishaji wa Mboji)

Inakadiriwa kuwa asilimia sabini (70%) ya kiasi cha taka ngumu zinazozalishwa nchini ni taka zinazoweza kurejelezwa. Hata hivyo, katika ya asilimia sabini (70%) ni asilimia tano hadi kumi (5-10%) pekee zinazorejelezwa na sekta isiyo rasmi. Viwango vya uzalishaji wa taka zinazoweza kurejelezwa vinatofautiana miongoni mwa majiji hapa nchini. Taka zinazorejelezwa kwa wingi ni pamoja na plastiki, karatasi, chuma chakavu, aluminiamu, glasi, taka za kielektroniki, betri za asidi chakavu na mafuta machafu.

Kwa miaka ya hivi karibuni, Tanzania imeendelea kuchukua hatua katika kuhamasisha urejelezaji wa taka. Mwaka 2022, kulikuwa na takribani kampuni 257 za urejelezaji wa taka na zaidi ya watu binafsi 99 walipewa vibali vya kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha ndani na nje ya nchi taka zinazoweza kutumika tena. Aidha, mwaka 2022 takriban tani 161,549 za taka ngumu zilisafirishwa nje ya nchi ikiwamo tani 7,389 za chuma chakavu.

Katika jitihada za kuhamasisha urejelezaji wa taka, Serikali imeandaa na kutekeleza Mwongozo wa Usimamizi wa Taka Ngumu kwa kutumia mbinu ya (Punguza, Tumia Tena na Rejeleza) wa Mwaka 2021. Aidha, Sekta binafsi na asasi za kiraia zimeendelea kutekeleza mwongozo huo ambapo baadhi ya viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazofungashwa kwenye vifungashio vya plastiki vimeungana pamoja katika kutekeleza Mpango wa Wajibu wa Wazalishaji wa Kusimamia Taka zinazotokana na bidhaa za wanzozalisha kwa kuondosha taka hizo kwenye Mazingira. Hivyo, hadi sasa kampuni nane za vinywaji zimeungana na kuunda chombo (PET PRO) cha kutekeleza Mpango huu wa usimamizi endelevu wa taka za plastiki. Chombo hiki kinalenga kukusanya na kurejeleza tani zaidi ya milioni 12.5 za taka za plastiki nchini kila mwaka.

Urejelezaji wa takaozo kupitia uzalishaji wa mboji ni mbinu muhimu ya usimamizi na udhibiti wa takaozo ambazo zinaweza kutumika katika shughuli za kilimo kwa kuwa husaidia kuongeza rutuba na unyevunyevu kwenye udongo. Aidha, teknolojia hii imeanza kutumika kwenye baadhi ya mikoa

kama vile Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na Pwani hivyo kusaidia kupunguza kiasi cha taka kinachopelekwa dampo.

Pamoja na kupunguza taka kwenye madampo, jitihada mbalimbali za kuzalisha nishati kutokana na taka zinaendelea kutekelezwa ambapo takriban Megawati kumi na tano (15) kwa mwaka huzalishwa katika viwanda vinne (4) vya sukari na pareto ambavyo ni Kilombero (Morogoro), Kagera sugar (Kagera), TPC Moshi (Kilimanjaro), na Taniwatt (Njombe).

### 5.2 Utupaji Salama wa Taka

Taka ngumu kutoka kwenye miji mara nyingi hutupwa kiholela, isipokuwa katika miji saba (7) yenye madampo ya kisasa. Miji hii ni pamoja na Arusha, Tanga, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Kigoma na Mtwara. Mahitaji ya ardhi kwa ajili ya utupaji salama wa taka yanaongezeka kwa kasi katika miji mikubwa, ambapo inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2030, takriban hekta 200 za ardhi zitahitajika kila mwaka kuhifadhi tani milioni 26 za taka. Hivyo ni muhimu kuhamasisha urejelezaji wa taka ngumu ili kupunguza kiasi cha taka kinachopelekwa dampo.

### 4.2 Usimamizi wa Majitaka

Kwa mujibu wa Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ya Mwaka 2024, kiasi cha majitaka kinachozalishwa nchini ni takriban lita za ujazo milioni 74 kwa mwaka, ikiwa ni sawa na wastani wa uzalishaji wa kati ya lita 120 na 180 kwa kila mtu kwa siku. Vyanzo vikuu vya uzalishaji wa majitaka ni pamoja na kaya, taasisi, maeneo ya biashara, masoko, viwanda na maji ya mvua. Usimamizi wa majitaka nchini hutumia mifumo ya kuhifadhi majitaka yanapozalishwa na/au kusafirishwa kupelekwa kwenye mabwawa mahususi ya kutibu majitaka. Vilevile, udhibiti wa majitaka ikiwamo mabwawa mahususi ya kutibu majitaka husimamiwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini.
Aidha, Mamlaka kumi na moja (11) kati ya themanini na tano (85) ndizo zenye mtandao wa ukusanyaji wa majitaka ikiwa ni asilimia 10.7% ambazo zimeunganisha takriban jumla ya wateja 56,899. Mfumo wa usimamizi wa majitaka huhusisha vyoo vya shimo na magari ya kubeba majitaka yanayosimamiwa na watoa huduma binafsi ya uondoshaji wa majitaka. Kwa ujumla, shughuli ya huduma ya uondoshaji wa majitaka katika miji mingi inatekelezwa kwa kiwango kidogo, isipokuwa katika jiji la Mwanza ambalo huduma ya uondoshaji wa majitaka ni sawa na asilimia 23.7. Ukuaji huu umetokana na kuongezeka kwa uunganishaji wa wateja wapya kwenye mtandao wa uondoshaji wa majitaka (Jedwali 2).

Pamoja na kuwapo kwa juhudi za kuunganisha wateja wapya bado uunganishaji huu hauendani na ongezeko la idadi ya watu na ukuaji wa miji. Katika maeneo ya mijini ambayo hayajaunganishwa kwenye mtandao Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, asilimia 42 wanatumia vyoo vilivyounganishwa na septiki tenki na asilimia 55 wanatumia vyoo vya kawaida vya shimo.

**Jedwali 2: Majiji yaliyo na mtandao wa uondoshaji wa majitaka kwa mwaka 2022/2023**

| Na. | Jina la Mamlaka | Urefu wa Mtandao(km) | Ulinganifu wa mtandao wa majitaka na |
|---|---|---|---|

| | | | jamii iliyounganishwa na mtandao (%) |
|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | 268.7 | 6.95 |
| 2 | DAWASA | 515.8 | 12.35 |
| 3 | Dodoma | 122.0 | 20.00 |
| 4 | Iringa | 80.3 | 6.80 |
| 5 | Mbeya | 138.0 | 14.00 |
| 6 | Morogoro | 43.6 | 6.71 |
| 7 | Moshi | 83.0 | 8.87 |
| 8 | Mwanza | 149.3 | 23.70 |
| 9 | Songea | 37.7 | 5.70 |
| 10 | Tabora | 24.7 | 4.59 |
| 11 | Tanga | 40.3 | 10.34 |

Chanzo: EWURA – Taarifa ya Utekelezaji (2022/23

### 5.2 Usimamizi wa Topekinyesi

Uondoshaji wa topekinyesi nchini unajumuisha matumizi ya magari 358 ya uondoshaji wa majitaka ambapo magari 41 yanamilikiwa na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira; 19 yanamilikwa na Halmashauri; na 298 yanamilikiwa na kampuni/watu binafsi. Mitambo ya kutibu majitaka ina uwezo wa kutibu kiasi cha majitaka lita za ujazo 179,295 kwa siku sawa na lita za ujazo 2,993,908 kwa mwaka. Kwa muktadha huo, kuna umuhimu wa kuongeza uwekezaji katika usimamizi wa topekinyesi ili kulinda afya ya binadamu na mazingira.

### 5.2 Usimamizi wa Maji ya Mvua

Usimamizi na udhibiti wa maji ya mvua ni suala muhimu katika kupunguza mafuriko, mmomonyoko wa ardhi na uchafuzi wa mazingira. Maji ya mvua hukusanywa kupitia mifereji iliyojengwa na mifereji ya asili iliyo kandokando ya barabara na yanaweza kutumika kama chanzo mbadala cha maji kwa matumizi mbalimbali. Hata hivyo, maji ya mvua bado yanakabiliwa na changamoto mbalimbali za ubora na upatikanaji wake.

Miundombinu kama vile mifereji, madaraja madogo na mabwawa ya kuhifadhi maji ya mvua kwa lengo la kuzuia mafuriko katika maeneo ya mijini husimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mamlaka ya Barabara Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, kampeni za elimu kwa umma ni muhimu katika kuhamasisha jamii kujenga tabia ya kutunza na kuzuia uchafuzi wa mifereji ya maji ya mvua. Ili kupunguza athari za mafuriko

yanayotokana na maji ya mvua, Serikali imefanya jitihada kubwa za kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za asili katika kuhifadhi ardhioevu na mifumo ya asili ya mifereji ya maji.

Aidha, nchi yetu imetenga takriban asilimia 10 ya ardhi yote kama ardhioevu; ambapo asilimia 5.5 ya eneo hilo imetambuliwa chini ya Mkataba wa Ramsar. Miongoni mwa maeneo hayo ni pamoja na Malagarasi/Muyovosi (Km² 32,500), Bonde la Ziwa Natron (Km² 2250), uwanda wa mafuriko wa Bonde la Kilombero (Km² 7,950) na Rufiji-Mafia-Kilwa (Km² 5,969.7). Kwa ujumla, maji ya mvua hukusanywa kutoka maeneo mbalimbali ya mijini na hayafanyiwi uchakataji wa kuyafanya yawe salama kabla ya kuingia kwenye vyanzo vya maji. Hali hii inasababisha maji hayo kuwa chanzo kikuu cha uchafuzi wa vyanzo vya maji.

Usimamizi wa maji ya mvua unaweza kuwa fursa kwa kugeuzwa kuwa chanzo cha maji iwapo maji hayo yatakusanywa, kuchakatwa na kutumika tena. Uvunaji wa maji ya mvua unaweza kuhamasishwa kwenye ngazi ya kaya na jamii kwa ujumla.

### 4.2 Tathmini ya Uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Usimamizi wa Taka

Kulingana na takwimu ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 uzalishaji taka ngumu ni kati ya tani 14-20.7 ambapo kati ya hizo, ni wastani wa asilimia 32.72 tu hukusanywa nchini kote. Aidha, miji mikuu hukusanya asilimia 63, na halmashauri za wilaya hukusanya asilimia 7.67 tu. Usimamizi usioridhisha wa taka ngumu kwenye halmashauri unachangiwa na changamoto mbalimbali ikiwa na pamoja na uwezo mdogo wa kitaasisi (fedha, watumishi, teknolojia); miundombinu hafifu; shughuli za usimamizi wa taka kutopewa kipaumbele; ushirikishwaji mdogo wa wadau; na mikataba ya uzoaji wa taka kutolewa kwa ya muda mfupi. Hali hii imechangia usimamizi hafifu wa taka.

Kumekuwapo na ongezeko kubwa la ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma ya usimamizi wa taka ngumu katika halmashauri nyingi nchini. Ongezeko hili limesaidia kupunguza gharama za utoaji wa huduma ya usimamizi wa taka ngumu ; kupunguza mzigo kwa Serikali za Mitaa ; na kuongeza maeneo ya ukusanyaji taka. Hata hivyo, imeonekana kumekuwapo na utendaji usioridhisha kwa baadhi makampuni ya usimamizi wa taka kunakosababishwa na mapato kidogo, matumizi ya vifaa duni vya ukusanyaji na usafirishaji wa taka na kutokuwapo kwa utaratibu mzuri wa uodoshaji wa taka. Aidha, utendaji usioridhisha umechangiwa na kutokuwa na mfumo madhubuti wa ukusanyaji wa ada za taka kunakochangia kushuka kwa ukusanyaji wa mapato. Pia, kutokuwapo na mifumo ya kuhamasisha shughuli za kuchakata taka, barabara zisizoweza kupitika kwa urahisi na usimamizi hafifu wa sheria ndogo za halmashauri kumechangia utendaji usioridhisha.

### 4.3 Ugharimiaji wa Shughuli za Usimamizi wa Taka

Ugharimiaji wa shughuli za usimamizi wa taka ni muhimu hususan katika uwekezaji wa miundombinu na uendeshaji wake. Utaratibu wa uendeshaji na ugharimiaji wa miundombinu ya usimamizi wa taka unatofautiana kati ya mji japokuwa chanzo kikuu ni mapato kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa, ada za watumiaji na michango kutoka sekta binafsi. Pamoja na kuwapo kwa juhudi za kuboresha mifumo hii ya ugharimiaji wa usimamizi wa taka, miji mingi bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa fedha, ukusanyaji mdogo wa mapato, na kutokuwapo kwa mapato lindwa ya usimamizi wa taka.

Takwimu zinaonyesha kuwa miji ya Mbeya, Tanga na Mwanza hupata ruzuku ndogo kutoka Serikali Kuu na hivyo kutegemea mapato ya ndani katika kutekeleza shughuli za usimamizi wa taka ngumu. Aidha, jiji la Arusha hutumia vyanzo vikuu vitatu ikiwa ni pamoja na ada ya huduma, adhabu kwa waliokiuka sheria, na ushirikiano na kampuni za sekta binafsi zinazohusika urejelezaji taka kwenye vituo vya Utenganishaji wa Taka (MRFs). Vilevile, Jiji la Tanga linakabiliwa na changamoto kubwa za kifedha kutokana na ukusanyaji mdogo wa mapato ambapo kiasi kinachokusanywa ni asilimia 56.5 ya bajeti iliyotakiwa kukusanywa na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa taka kwa ufanisi. Kwa muktadha huo, ni muhimu kubuni vyanzo zaidi vya mapato na kuwa na mfumo madhubuti wa ugharimiaji wa shughuli za usimamizi wa taka ili kuhakikisha usimamizi endelevu wa taka nchini.

### 4.4 Jinsia katika Usimamizi wa Taka

Katika maeneo mengi ya miji, vikundi vya kijamii vinavyojihusisha na ukusanyaji wa taka ngumu vinashirikisha wanaume, wanawake, na vijana. Muundo wa uendeshaji wa vikundi hivi, mara nyingi nafasi ya uenyekiti huchaguliwa mwanamke. Katika sekta ya urejelezaji wa taka, wanawake hushughulikia zaidi uchambuaji na utenganishaji wa taka, wakati wanaume hufanya kazi zinazohitaji kutumia nguvu kama vile kupakia taka kwenye magari ya taka. Aidha, katika shughuli za usimamizi wa taka, takwimu zinaonesha kuwa ushiriki wa wanawake ni mkubwa kuliko wanaume. Mathalani, katika mkoa wa Mbeya ushiriki wa wanawake ni 72% na Mkoa wa Mwanza ni 54%, ikilinganishwa na wanaume ambao ni 28% na 46% mtawalia. Aidha, zaidi ya 50% ya wadau wanaohusika katika shughuli za kufanya usafi wa barabara ni wanawake.

### 4.5 Kukuza uelewa kwa umma, ushirikishwaji wa jamii na Sekta Binafsi

Kukuza uelewa kwa umma na ushirikishwaji wa jamii na sekta binafsi ni suala muhimu katika kuhamasisha jamii kubadili tabia katika usimamizi bora wa taka. Kwa miaka mingi, Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, taasisi za elimu, vyombo vya habari na asasi zisizo za serikali zimekuwa zikishiriki kikamilifu katika kukuza uelewa wa umma kuhusu usimamizi endelevu wa taka. Hatua mbalimbali zimetumika katika kukuza uelewa na ushiriki wa jamii kupitia ziara za nyumba kwa nyumba; uhamasishaji wa jamii ikiwamo wanawake, vijana na wanafunzi; kushiriki zoezi la usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi; na mashindano ya kitaifa ya kila mwaka ya usafi wa mazingira.

Hata hivyo, pamoja na jitihada hizi, uelewa wa jumla wa umma kuhusu masuala ya usimamizi endelevu wa taka miongoni mwa wadau wote nchini bado ni mdogo. Hali hii inachangiwa na mtazamo wa jamii kuwa usimamizi wa taka ni jukumu la mamlaka za serikali za mitaa, ukosefu wa rasilimali za kiufundi na kifedha, pamoja na viwango tofauti vya uelewa katika kusaidia usimamizi endelevu wa taka.
Inatarajiwa kuwa kadiri jamii inavyohamasika na kushiriki kikamilifu, ndivyo itakavyokuwa tayari zaidi kuchukua jukumu la kuboresha usimamizi wa taka.

### 4.6 Changamoto na Fursa

### 5.2 Changamoto

Changamoto za udhibiti na usimamizi wa taka nchini ni pamoja na:

**Uhaba wa Takwimu**
Shughuli za usimamizi wa taka zinakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na utaratibu sahihi wa ukusanyaji wa takwimu kunakoathiri uandaaji wa mipango na utekelezaji wa mikakati ya udhibiti wa taka nchini.

**Ugharimiaji usio madhubuti wa usimamizi wa taka**
Ugharimiaji wa usimamizi wa taka ni mojawapo ya changamoto inayoikabili sekta ya usimamizi wa taka nchini. Majiji na manispaa huwa na vipaumbele vingi vinavyohitaji rasilimali fedha, kama vile elimu, huduma za afya, miundombinu ya maji na barabara. Kuwapo kwa vipaumbele vingi husababisha shughuli za usimamizi wa taka kutopewa kipaumbele. Hivyo, ni muhimu fedha za shughuli za usimamizi wa taka kuwa mapato lindwa ili yatumike moja kwa moja katika shughuli za usimamizi wa taka.

**Utenganishaji hafifu wa taka**
Pamoja na kuwa Sekta zisizo rasmi zinajihusisha na shughuli za usimamizi wa taka bado utenganishaji wa taka katika vyanzo unakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo kutokuwa na ujuzi wa kutosha na upungufu wa vituo vya kuchakata na kurejeleza taka.

**Miundombinu duni ya utupaji taka**
Miji mingi haina magari maalum na vitendea kazi vya usimamizi wa taka. Aidha, kaya nyingi hutumia vyombo vya kuhifadhia taka visivyo na viwango kama vile mapipa, mifuko ya karatasi, mifuko ya plastiki, makasha ya takataka, ndoo, au magunia ambavyo husababisha baadhi ya taka kurudi kwenye mazingira.

**Kutokuwapo kwa Mfumo wa Kidijitali wa Usimamizi wa Takwimu za Taka**
Tanzania inakabiliwa na ukosefu wa mfumo wa kidijitali wa ukusanyaji wa takwimu za usimamizi wa taka. Hali hii imesababisha kukosekana kwa takwimu na hivyo kuathiri mipango na utekelezaji wa mikakati madhubuti ya udhibiti na usimamizi wa taka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Kutokuwa na mamlaka ya usimamizi wa taka**
Kukosekana kwa mamlaka moja ya kusimamia taka kumesababisha kuwapo kwa taasisi nyingi zinazoingiliana kimajukumu katika usimamizi wa taka na kusababisha huduma hafifu katika usimamizi wa taka.

**Upungufu wa Vituo na Viwanda vya kuchakata na kurejeleza taka**
Tanzania ina vituo na viwanda vichache vyenye teknolojia inayoweza kuchakata na kurejeleza baadhi ya taka. Hali hii, imesababisha taka nyingi kupelekwa dampo au kubakia katika maeneo zinakozalishwa.

## 5.2 Fursa
Usimamizi wa taka nchini una fursa mbalimbali ambazo ni pamoja na:

**Sera na sheria wezeshi za usimamizi wa taka**
Kuwapo kwa sera na sheria wezeshi ambazo zinatoa miongozo ya jumla inayoelekeza kupunguza uzalishaji wa taka, uwekezaji katika urejelezaji wa taka na ushirikishwaji wa sekta binafsi.

**Urasimishaji wa sekta zisizo rasmi katika usimamizi wa taka**
Sekta ya usimamizi wa taka nchini inatoa fursa kwa sekta zisizo rasmi kushiriki shughuli za ukusanyaji na urejelezaji wa taka. Urasimishaji wa sekta zisizo rasmi ikiwamo wakusanya taka utachangia kuimarisha usimamizi wa taka katika maeneo mbalimbali nchini.

**Ushirikishwaji wa jamii**
Jamii ni miongoni mwa wadau wa uzalishaji wa taka, hivyo ina fursa ya kushiriki katika shughuli za udhibiti na usimamizi wa taka nchini kwa kuhamasisha kupunguza uzalishaji na urejelezaji wa taka ili kuongeza kipato, kulinda afya ya jamii na mazingira.

**Ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi**
Usimamizi wa taka unatoa fursa kwa sekta binafsi kushirikiana na Serikali katika uwekezaji wa usimamizi wa taka ikiwamo zabuni za ukusanyaji wa taka, kuwekeza katika vituo na viwanda vya kurejeleza taka.

**Utafiti, elimu na teknolojia**
Taasisi za elimu na utafiti zina fursa ya kufanya utafiti na kubuni teknolojia zitakazoimarisha usimamizi wa taka.

**Utekelezaji wa mbinu jumuishi ya usimamizi wa topekinyesi na maji ya mvua**
Kuwapo kwa mbinu jumuishi kutatoa fursa ya kuimarisha usimamizi wa majitaka hususan katika matumizi ya taka ili kuzalisha nishati, kuchakata taka na kutumia tena majitaka yaliyorejelezwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwamo kilimo.

# SURA YA TANO: MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI

Sura hii inahusu hatua za kipaumbele za kuboresha mbinu za sasa za usimamizi wa taka kwa kuzingatia changamoto na fursa zilizobainishwa. Lengo kuu la mpango ni kuimarisha usimamizi endelevu wa taka kupitia dhana ya uchumi rejeshi.

## 5.2 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

### 5.12.1 Kuimarisha Upunguzaji wa Taka Kupitia Dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza

Ili kupunguza taka kupitia dhana ya punguza, tumia tena, na rejeleza, Tanzania inapaswa kuweka vipaumbele vya kutekeleza mikakati ya kiudhibiti ili kufanikisha dhana ya uchumi rejeshi usio na kiwango kikubwa cha uzalishaji wa taka. Mikakati hii ni pamoja na programu za utenganishaji taka; kuimarisha Vituo vya Utengenishaji wa Taka (MRF); kuanzisha shughuli za kutengeneza mboji kutokana na takaozo (taka zinazotokana na viumbe hai); kutumia taka kuzalisha nishati; na kuanzisha vituo vya kimkakati vya kuchakata taka za kielektroniki. Upunguzaji wa taka unasaidia katika kuhifadhi rasilimali, kuhifadhi mazingira, kupunguza hewa ukaa, kutunza afya ya umma, na kupunguza gharama za ukusanyaji na usafirishaji wa taka.

### 5.2 Kuimarisha utenganishaji wa taka

Ili kuimarisha utenganishaji wa taka, mkakati madhubuti utaanzishwa katika miji, manispaa na maeneo ya miji midogo. Mikakati hii itajumuisha kampeni za uhamasishaji kwa jamii ili kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutenganisha taka, kwa lengo la kufikia angalau asilimia 50 ya kaya katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa. Aidha, warsha zitakazotolewa zitaekeza mbinu sahihi za kutenganisha takaozo, taka zinazoweza kurejelezwa, taka hatarishi, na taka nyinginezo. Ili kutekeleza jitihada hizi, kaya na taasisi zitapewa elimu ya kutumia mapipa ya taka yenye rangi tofauti kwa ajili ya kutofautisha taka za kikaboni, taka za kurejelezwa, na taka nyinginezo katika kaya, shule, hospitali, masoko, na ofisi za umma ili kurahisisha na kuimarisha utenganishaji endelevu wa taka.

### 5.2 Kuanzisha na kuimarisha vituo vya utengenishaji wa taka

Vituo vya Utenganishaji wa Taka, vinavyojulikana pia kama mitambo ya uchakataji wa taka, vimeundwa kwa ajili ya kuzalisha malighafi safi, zenye ubora wa juu, ambazo zinaweza kuuzwa na kuwa na thamani nzuri kiuchumi. Mkakati huu unalenga kuanzisha na kuimarisha MRF ili kuboresha utenganishaji wa taka, kuongeza kiwango cha urejelezaji, kupunguza matumizi ya madampo, na kusaidia katika kufanikisha malengo ya uchumi rejeshi.

Angalau kituo kimoja cha kutenganisha taka kitajengwa na kuanza kufanya kazi katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kila kituo kitakuwa na vifaa kwa ajili ya kuchambua, kupima, kufungasha, na kuhifadhi kwa muda zinazoweza kurejelezwa. Mkakati huu pia unajumuisha ujenzi wa kituo kimoja (1) cha uchakataji wa awali ambacho kitafanya kazi ya kupokea taka na kuziandaa ikiwamo kuzitenganisha, kuzisafisha au kuzisaga kabla ya kupelekwa katika vituo vya utenganishaji wa taka kwa ajili ya kuchakatwa zaidi.

Ili kuimarisha uendelevu na ufanisi, mkakati huu utafungua fursa kwa sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu, kuendesha vituo vya utenganishaji taka na vituo vya awali vya uchakataji, au kuuza malighafi zilizozalishwa. Njia hii inalenga kuboresha ufanisi wa kiutendaji, kupunguza mzigo wa gharama kwa serikali, na kuchochea maendeleo ya uchumi wa kijani nchini.

### 5.2 Kuanzisha na/au kuimarisha vituo vya uzalishaji wa mboji

Tanzania hutumia mbinu za kutengeneza mboji kwa kuvundika takaozo na kuzalisha finyufinyu (Black Soldier Fly), kubadilisha takaozo kuwa bidhaa tofauti, kama vile mboji, na vyakula vya mifugo. Mkakati utajikita katika kujenga angalau mtambo mmoja katika kila mamlaka ya serikali ya mtaa kwa kutumia teknolojia zote mbili zinazopatikana nchini. Lengo kuu ni kuzalisha mboji zenye ubora na kupunguza athari hasi zinazoweza kutokana na utupaji usiofaa wa taka za kikaboni.

### 5.2 Kuanzisha kituo cha kuzalisha nishati kwa kutumia taka

Kubadilisha taka kuwa nishati kunahusisha kuchoma taka katika mazingira yaliyo salama na yaliyo na udhibiti maalum wa hewa chafu, ili kupata joto la kutumia kuzalisha nishati. Mchakato huu unahusisha kuchoma taka ili kupata joto (na mvuke), ambalo hutumika kuzalisha umeme. Mkakati utajenga angalau mradi mmoja (1) wa majaribio wa kituo cha kubadilisha taka kuwa nishati, kitakachowekewa mifumo ya kudhibiti uchafuzi wa hewa, katika mojawapo ya miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Arusha, Tanga, au Morogoro.

### 5.2 Kuanzisha au kuboresha vituo vya mwisho vya utupaji wa Taka

Mkakati huu unalenga kujenga au kuboresha angalau dampo la kisasa moja (1) katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA) kwa ajili ya kushughulikia taka zisizoweza kurejelezwa zinazotoka katika vituo vya awali vya uchakataji taka kama vile Vituo vya Utengenishaji Taka, vituo vya kuzalisha mboji, shughuli za kuchakataji wa taka, na mitambo ya kubadilisha taka kuwa nishati.

Lengo ni kupunguza athari kwa mazingira na afya ya jamii, sambamba na kufanikisha malengo ya kitaifa ya usimamizi jumuishi wa taka ngumu.

### 5.17.1 Kuimarisha Usimamizi wa Taka

### 5.2 Kuimarisha ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi wa taka

Ili kuongeza ushiriki na ushirikiano wa wadau wote wanaohusika katika upangaji, uendelezaji, na usimamizi wa miundombinu ya taka, kwa kuhakikisha kuwa mbinu za usimamizi wa taka zinakuwa endelevu na jumuishi. Mkakati huu unalenga kuongeza ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi wa taka kwa angalau asilimia 10 kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

### 5.18.1 Kuimarisha Usimamizi Endelevu wa Majitaka

Mkakati huu unahimiza usimamizi endelevu wa majitaka na maji ya mvua, kwa kuzingatia zaidi kuzuia, kutumia tena, au kurejeleza.

### 5.2 Usimamizi wa majitaka na takakinyesi

Mkakati unapendekeza hatua mbalimbali zenye lengo la kufikia hali ya kutokuwa na taka kabisa katika maeneo ya uzalishaji wa majitaka na takakinyesi. Mkakati huu unahimiza yafuatayo:

### 5.2 Kukuza na kuweka mifumo madhubuti na endelevu ya teknolojia za kutibu majitaka na takakinyesi

Mbali na teknolojia za kawaida kama mabwawa ya kutibu majitaka, mkakati huu unasisitiza kutumia teknolojia za kutibu kwa kutumia teknolojia isiyotumia hewa/teknolojia inayotumia bakteria (Anaerobic treatment technologies) yenye uwezo wa kuchakata taka ngumu, takaozo na majitaka, katika ngazi za kaya na jamii/manispaa. Aidha, teknolojia hizi zinalenga urejelezaji na uzalishaji wa rasilimali kama vile uzalishaji wa biogesi, mbolea zitokanazo na takaozo, na maji safi yanayoweza kutumika tena. Kwa hiyo, mkakati unalenga kuhamasisha angalau asilimia 50 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha na kutumia teknolojia hizi.

### 5.2 Kuimarisha programu za matumizi ya majitaka

Mkakati unatambua kuwapo kwa matumizi ya majitaka yaliyowekwa dawa hapa Tanzania. Hata hivyo, majitaka yaliyorejelezwa hutumika kwa kiwango kidogo sana. Mkakati huu unajielekeza katika kuchunguza fursa za kutumia tena majitaka yaliyo chakatwa kwa ajili ya umwagiliaji, shughuli za viwandani, upandaji nyasi na miti katika maeneo ya mijini, mitambo umwagiliaji, kurejesha maji ardhini, kusafisha vyoo, au matumizi mengine yasiyohusisha kunywa. Mkakati unalenga kuhakikisha kuwa angalau asilimia 20 ya majitaka yaliyochakatwa yanatumika.

### 5.2 Kuimarisha mifumo midogo ya uchakataji majitaka (DEWATS)

Mfumo wa DEWATS una faida nyingi ikilinganishwa na mifumo ya kawaida ya majitaka na ile ya kumwaga majitaka mwisho wa bomba, zikiwamo gharama ndogo za uwekezaji, uwezo wa kurejeleza rasilimali, na uwezo wa kushughulikia taka tofauti kwa pamoja.

Ili kufikia hali ya kutokuwa na taka na kutokomeza uchafuzi wa mazingira katika hatua zote za uzalishaji wa taka, mkakati unasisitiza umuhimu wa kuanzisha na kutumia mfumo wa DEWATS, kwa pamoja na mfumo rahisi wa usafirishaji wa majitaka kwa pamoja kwa makazi ya pamoja katika maeneo ya mijini na vijijini. Mkakati unatarajia kuwa na angalau mfumo mmoja wa DEWATS katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA).

### 5.3 Usimamizi wa Maji ya Mvua

Mkakati unalenga kulinda ubora wa maji na kupunguza athari hasi za maji yanayotiririka kwa kudhibiti kiasi na ubora wa maji ya mvua yanayoingia kwenye njia za maji. Mkakati huu utafanikishwa kwa kutoa elimu kwa umma pamoja na kutumia mbinu bora za usimamizi, na hatua za kiudhibiti.

### 5.2 Kukuza usimamizi wa maji ya mvua

Mkakati huu unalenga kuboresha na kuanzisha hatua za udhibiti wa maji ya mvua, ikijumuisha uvunaji wa maji ya mvua katika ngazi ya kaya, taasisi na jamii kwa ujumla. Pia, unahimiza ukusanyaji na uhifadhi wa maji ya mvua yanayotiririka ardhini kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile umwagiliaji, kunywesha mifugo, na mabwawa ya mapumziko katika mazingira ya mijini na vijijini. Mkakati unasisitiza kuzuia uchafu kuingia kwenye maji ya mvua yanayotiririka ardhini, kwa mfano kupitia utupaji sahihi wa taka na usafi wa mara kwa mara wa miundombinu inayotumika kutiririsha maji ya mvua. Mkakati utahamasisha matumizi ya teknolojia za uvunaji wa maji ya mvua kwa asilimia 30 ya kaya na taasisi katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa. Vilevile, mkakati utahamasisha uwekaji

dawa maji ya mvua na miundombinu ya utunzaji mazingira kwa ajili ya kuongeza uhimilivu wa miji dhidi ya mafuriko.

### 5.2 Kuimarisha usafi wa miundombinu ya maji ya mvua

Mifereji ya maji imekuwa ikizidiwa na taka ngumu kutokana na usimamizi duni wa taka ngumu katika miji mingi. Utupaji wa taka ngumu kwenye mifereji ya maji husababisha kuziba kwa mifereji hiyo na hatimaye kusababisha mafuriko. Mkakati unahimiza usafi wa mara kwa mara wa miundombinu ya mifereji ya maji kwa kuzingatia kanuni za kitaifa zinazohusika pamoja na sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA). Mkakati utahamasisha utekelezaji wa usafi wa mifereji kwa kiwango cha angalau asilimia 80 ya mifereji yote katika LGAs zote.

### 5.24.1 Kuimarisha uwezo wa kitaasisi na Mfumo wa usimamizi wa Taka

### 5.2 Kuimarisha mfumo wa ugharimiaji usimamizi wa taka

Majiji na halmashauri zina jukumu kuu la kugharimia shughuli za usimamizi wa taka, ambapo asilimia 70 ya fedha huelekezwa katika uendeshaji na matengenezo. Kutokana na jukumu hilo kuna haja ya kuimarisha mifumo na mipango ya kifedha ya serikali za mitaa inayohakikisha upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya magari ya ukusanyaji taka na motisha kwa vikundi vya kijamii ili kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa taka, pamoja na uwekezaji katika vituo vya utenganishaji wa taka na uboreshaji wa miundombinu ya taka. Vilevile, sekta binafsi inaweza kushiriki katika uwekezaji pale ambapo kuna fursa za kupata faida na njia za kurejesha gharama.

### 5.2 Kuimarisha utekelezaji wa nyenzo za usimamizi wa taka

Utekelezaji madhubuti wa nyenzo za usimamizi wa taka ni muhimu katika kufanikisha usimamizi endelevu wa taka. Mkakati huu unalenga kuboresha uzingatiaji na utekelezaji wa nyezo za usimamizi wa taka kama vile mipango, miongozo na sheria ndogo kwa angalau asilimia 50 kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa, Kata hadi Halmashauri.

### 5.2 Kurasimisha wakusanyaji taka

Sekta isiyo rasmi (wakusanyaji taka, wakusanya vyuma chakavu, wafanyabiashara na warejelezaji) ina mchango mkubwa katika usimamizi wa taka ngumu za majiji na manispaa na kupunguza gharama za ukusanyaji kwa kufanya urejelezaji. Licha ya mchango wao mkubwa, mara nyingi hawatambuliki rasmi. Mkakati huu unalenga kurasimisha wakusanyaji taka ili kuboresha mazingira yao ya kazi, kuwawezesha kupata mikopo ya kifedha na kuunganishwa kwenye minyororo ya masoko.

### 5.2 Kuimarisha utafiti na kusambaza teknolojia bunifu

Mbinu za usimamizi wa taka zimefungamana na utafiti kuhusu ujumuishaji wa teknolojia bunifu katika sekta ya usimamizi wa taka. Kuna ongezeko la mahitaji ya teknolojia bunifu zinazopunguza vihatarishi vya kiafya kwa mazingira, kuongeza ufanisi wa gharama, na kuonyesha ufanisi wa kutumika kwa kiwango kikubwa. Hivyo basi, mkakati unalenga kusambaza matokeo ya tafiti bunifu kupitia mkutano wa mwaka kwa kushirikisha taasisi za elimu ya juu, wataalamu, sekta binafsi na taasisi za utafiti.

### 5.2 Kukuza Uelewa wa Umma, Ushirikishwaji wa Jamii na Sekta Binafsi

**Kuimarisha utekelezaji wa siku ya usafi Kitaifa**

Mkakati huu umeandaliwa kuhakikisha kuwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA) inatekeleza Siku ya Usafi Kitaifa (kila Jumamosi ya mwiso wa mwezi). Aidha, mkakati utaongeza kasi ya utekelezaji wa mbinu bunifu zilizopo zinazochangia utumiaji tena, urejeleaji, na urejelezaji.

**Kukuza uelewa wa umma**

Kuna kiwango kidogo cha uelewa wa jamii kuhusu usimamizi wa taka, ikiwa ni pamoja na utenganishaji wa taka katika chanzo, ushughulikiaji sahihi wa taka, na urejelezaji. Hivyo, kuna haja ya kubuni, kuandaa na kusambaza taarifa kwa njia sahihi kwa ajili ya elimu na uhamasishaji wa jamii kuhusu usimamizi wa taka. Lengo la mkakati ni kuhakikisha kuwa angalau asilimia 30 ya wadau wanakuwa na uelewa kuhusu mbinu bora za usimamizi wa taka zinazochochea urejelezaji, na hivyo kuchangia katika mabadiliko ya tabia.

**Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi**

Utekelezaji madhubuti wa usimamizi wa taka unahitaji ushiriki wa moja kwa moja wa sekta binafsi katika nyanja za ubunifu na uongezaji thamani kwenye michakato ya usimamizi wa taka. Mkakati huu unalenga kuihusisha sekta binafsi kuanzia hatua ya upangaji kwa kubuni na kutekeleza uwekezaji ambao ni suluhisho la usimamizi jumuishi wa taka. Jitihada hizi zitaboresha ukusanyaji, usafirishaji, na urejeleaji wa taka. Lengo ni kuhakikisha kuwa angalau asilimia 50 ya taka zinazozalishwa zinasimamiwa kwa ushirikiano na sekta binafsi, kwa kuhimiza ushiriki wao katika uwekezaji na ubunifu wa usimamizi wa taka, ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kusimamia vituo vya kuchakata na kurejeleza-taka

**Jedwali 3: Mkakati wa Utekelezaji**

| **Shughuli** | **Maeneo ya Kipaumbele** | **Shabaha** | **Kiashiria** | **Njia za uthibitishaji** | **Muda wa utekelezaji** | Makadirio ya bajeti (TShs 'Bilioni) | **Mhusika** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Lengo la Kimkakati 1: Kuimarisha Upunguzaji wa Taka kupitia dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza** | | | | | | | |
| Kuimarisha utenganishaji wa taka | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | 50% ya Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Idadi ya kaya zinazotenganisha taka | Ripoti | 2025-2027 | 0.8 | OR-TAMISEMI, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa |
| Kuimarisha utenganishaji na uchambuaji wa taka katika vituo na taasisi za kukusanyia taka | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | 50% ya taasisi zenye mifumo ya utengenishaji | Idadi ya vituo vya uchambuaji taka vilivyofanyiwa majaribio | Ripoti | 2025-2027 | | OR-TAMISEMI, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa |
| Kufanya kanpeni ya uelimishaji umma kuhusu utenganishaji taka | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | 50% ya Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zilizofikiwa | Idadi ya kampeni za umma zilizofanyika | Ripoti | 2025-2027 | | OR-TAMISEMI, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa |
| Kutoa mwongozo wa kitaalamu na maelekezo kuhusu matumizi ya rangi maalum katika utenganishaji wa | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau 80% ya taasisi zilizoshiriki | Asilimia ya watu katika Mamlaka za Serikali za | Ripoti | 2025-2027 | | OR-TAMISEMI, Mamlaka zote za Serikali za |

| Shughuli | Maeneo ya Kipaumbele | Shabaha | Kiashiria | Njia za uthibitishaji | Muda wa utekelezaji | Makadirio ya bajeti (TShs 'Bilioni) | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| taka | | | Mitaa wanaotenga taka kwa kutumia rangi | | | | Mitaa |
| **5.2 Kuanzisha na kuimarisha vituo vya utengenishaji wa taka** | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau MRF (1) katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa | Idadi ya MRF zilizoanzishwa | Ripoti | 2025-2027 | 0.25 | OR-TAMISEMI, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa |
| Kuanzisha na kuimarisha vituo vya uchakataji | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau kituo (1)cha uchakataji wa awali katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa | Idadi ya vituo vya uchakataji wa awali | Ripoti | 2025-2027 | 0.25 | OR-TAMISEMI, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa |
| Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika urejelezaji | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau 10% ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizoshirikisha sekta binafsi | Idadi ya makubaliano rasmi yaliyoanzishwa | Ripoti | 2025-2027 | 0.25 | OR-TAMISEMI, NEMC, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa, |
| Kuanzisha na/au kuimarisha vituo vya uzalishaji wa mboji | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau kituo (1) cha kuzalisha mboji katika kila Mamlaka zote za | Idadi ya vituo vya kuzalisha mboji vilivyoanzishwa | Ripoti | 2025-2027 | 0.5 | OR-TAMISEMI, NEMC, Mamlaka zote |

| Shughuli | Maeneo ya Kipaumbele | Shabaha | Kiashiria | Njia za uthibitishaji | Muda wa utekelezaji | Makadirio ya bajeti (TShs 'Bilioni) | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Serikali za Mitaa | | | | | za Serikali |
| Kuanzisha kituo cha kuzalisha nishati kwa kutumia taka | Majiji ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Dodoma na/au Manispaa ya Morogoro | Angalau kituo (1) cha kubadili taka kuwa nishati kuanzishwa | Idadi ya vituo vya kubadili taka kuwa nishati vilivyoanzishwa | Ripoti | 2025-2027 | 0.6 | OR-TAMISEMI,, MIIT, MoH, NEMC, Dar es Salaam, Mbeya,Mwanza ,Dodoma na Morogoro |
| Kuanzisha au kuboresha vituo vya mwisho vya utupaji wa Taka | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau dampo moja kujengwa au kuimarishwa | Idadi ya madampo yaliyoanzishwa | Ripoti | 2025-2030 | 20 | OR-TAMISEMI, NEMC, Mamlaka zote za Serikali |
| **Jumla Ndogo** | | | | | | **3.15** | |
| **Lengo la Kimkakati 2: Kuimarisha Ushughulikiaji wa Taka** | | | | | | | |
| Kuimarisha Ushirikishwaji wa Wadau katika Usimamizi wa | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau 10% ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | Idadi ya wadau walioshirikishwa | Ripoti | 2025-2030 | 0.25 | OR-TAMISEMI, Mamlaka zote |

| Shughuli | Maeneo ya Kipaumbele | Shabaha | Kiashiria | Njia za uthibitishaji | Muda wa utekelezaji | Makadirio ya bajeti (TShs 'Bilioni) | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Taka | | kushirikisha wadau katika usimamizi wa taka | | | | | za Serikali za Mitaa |
| **Jumla Ndogo** | | | | | | **56.5** | |
| **Lengo la Kimkakati 3: Kuimarisha usimamizi endelevu wa majitaka** | | | | | | | |
| Kutenga na kuweka mipaka ya maeneo ya kutosha ya ardhi kwa ajili ya miundombinu ya usimamizi wa taka ili kukidhi mahitaji ya muda mrefu. | Halmashauri zote | Angalau Hekta 80 kutengwa na kuwekwa mipaka kwa 20% halmashauri | Idadi ya hekta zilizotengwa na kuwekwa mipaka | Ripoti | 2025-2030 | 92 | OR-TAMISEMI, MLHHSD, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa, |
| Kujenga au kuboresha mitambo ya kusafisha majitaka na mabwawa ya majitaka. | Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Kibaha, Babati | Mitambo na mabwawa ya majitaka. 6 kujengwa | Idadi ya mitambo ya kuchakata majitaka iliyoanzishwa au kuboreshwa | Ripoti | 2025-2030 | 240 | **MoW,** OMR, MoH, NEMC, Bodi za Usimamizi wa Mambonde ya maji,<br>Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Morogoro, |

| Shughuli | Maeneo ya Kipaumbele | Shabaha | Kiashiria | Njia za uthibitishaji | Muda wa utekelezaji | Makadirio ya bajeti (TShs 'Bilioni) | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | Kibaha, Babati |
| Kukuza matumizi ya teknolojia madhubuti na endelevu za kutibu majitaka na topekinyesi. | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau 50% ya mamlaka za serikali za mitaa zitatumia teknolojia ya kuchakata topekinyesi. | Idadi ya mitambo ya kitibu majitaka | Ripoti | 2025-2030 | | **MoW,** OMR, MoH, NEMC, Bodi za Usimamizi wa Mambonde ya maji. |
| Kuimarisha program za urejelezaji majitaka | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau 20% majitaka yaliyorejelezwa kutumika tena. | Idadi programu | Ripoti | 2025-2030 | | **MoW,** OMR, MoH, NEMC, Bodi za Usimamizi wa Mambonde ya maji |
| **5.2 Kukuza matumizi ya mifumo midogo ya uchakataji majitaka** | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau DEWATS (1) kutumika katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Idadi ya DEWATS | Ripoti | 2025-2030 | | **MoW,** OMR, MoH, NEMC, Bodi za Usimamizi wa Mambonde ya maji |
| Kuimarisha usimamizi wa maji ya mvua | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau 30% ya kaya na taasisi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia | Idadi ya kaya | Ripoti | 2025-2030 | | **MoW,** OMR, MoH, NEMC, Bodi za Usimamizi wa |

| Shughuli | Maeneo ya Kipaumbele | Shabaha | Kiashiria | Njia za uthibitishaji | Muda wa utekelezaji | Makadirio ya bajeti (TShs 'Bilioni) | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | teknolojia za kusimamia maji ya mvua | | | | | Mambonde |
| Kuimarisha usafi wa miundombinu ya maji ya mvua | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau 80% ya mitaro kusafishwa katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Asilimia ya mitaro iliyosafishwa | Ripoti | 2025-2030 | | **MoW,** OMR, MoH, NEMC, Bodi za Usimamizi wa Mambonde |
| **Jumla Ndogo** | | | | | | **352** | |
| **Lengo la Kimkakati 4: Kuimarisha uwezo wa kitaasisi na Mfumo wa usimamizi wa Taka** | | | | | | | |
| **5.2 Kuboresha mfumo wa ugharimiaji usimamizi wa taka** | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Idadi ya halmashauri zilizofanyiwa tathmini | Ripoti | 2025-2027 | 2.2 | OR-TAMISEMI, MoFP, OMR, MoH |
| **5.2 Kuimarisha utekelezaji wa nyenzo za usimamizi wa taka** | Kijiji/Mtaa, kata na Mamlaka za Serikali za Mitaa | 50% ya Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Idaadi ya mipango, miongozo, na sheria ndogo zilizoandaliwa na kutekelezwa | Mipango, miongozo, na sheria ndogo | 2025-2027 | 0.92 | OR-TAMISEMI, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa |
| Kushirikisha sekta isiyo rasmi katika usimamizi wa taka | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau 50% ya sekta zisizo rasmi kurasimishwa | Idadi ya sekta zisizo rasmi zilizorasmishwa | Rejista | 2025-2030 | 1.34 | OR-TAMISEMI, OMR, NEMC, Mamlaka zote |

| Shughuli | Maeneo ya Kipaumbele | Shabaha | Kiashiria | Njia za uthibitishaji | Muda wa utekelezaji | Makadirio ya bajeti (TShs 'Bilioni) | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ifikapo 2030 | | | | | za Serikali za Mitaa |
| Kuimarisha utafiti na kusambaza teknolojia bunifu | Nchi nzima | Taasisi za elimu, wataalamu na sekta binafsi, taasisi za utafiti na asasi zingine. | Idadi ya mikutano ya kila mwaka ya usimamizi wa taka | Idadi ya wadau walioshiriki | 2025-2030 | 0.92 | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa, Halmashauri |
| Kuimarisha kamati za usimamizi wa taka katika ngazi ya kata, kijiji na mtaa | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Angalau 80% katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Idadi ya wafanyakazi walioajiriwa au kuteuliwa | Mikataba | 2025-2030 | 8.2 | OR-TAMISEMI, Utumishi wa Umma, Mamlaka zote za Serikali za Mitaa, |
| Kuanzisha mfumo wa taarifa za usimamizi wa taka. | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Mifumo ya taarifa ya usimamizi wa taka kuanzishwa | Idadi ya mifumo ya taarifa ya usimamizi wa taka iliyoanzishwa | Kuwapo kwa mfumo wa usimamizi wa taarifa | 2025-2027 | 0.1 | OR-TAMISEMI, ORM, MoH, NEMC, eGA |
| Kumarisha ufuatiliaji na hatua za utekelezaji wa usimamizi wa taka. | Halmashauri zote | Angalau 20% ya mifumo ya usimamizi wa taka inakaguliwa na kufuatiliwa | Idadi ya nyezo zilizotekelezwa | Ripoti | 2025-2030 | 0.2 | MoW, MoH, Bodi ya Usimamizi wa Mabonde ya Maji, NEMC, |

| Shughuli | Maeneo ya Kipaumbele | Shabaha | Kiashiria | Njia za uthibitishaji | Muda wa utekelezaji | Makadirio ya bajeti (TShs 'Bilioni) | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | Halmashauri zote |
| Kufanya ufatiliaji na tathmini ya mkakati | Halmashauri zote | Angalau 80% ya shughuli zote zilizopangwa zimetekelezwa | Idadi ya shughuli zilizotekelezwa | Ripoti | 2025-2030 | 1 | ORM, OR-TAMISEMI, MoH, Mamalaka za Serikaliza Mitaa |
| | | | | | | | |
| **Lengo la Kimkakati 5: Kukuza Uelewa wa Umma, Ushirikishwaji wa Jamii na Sekta Binafsi** | | | | | | | |
| Kuimarisha ushiriki wa jamii katika siku ya usafi Kitaifa | Halmashauri zote | 20% ya halmashauri kushiriki siku ya usafi Kitaifa | Idadi ya Halmashauri | Ripoti | 2025-2030 | 0.2 | OR-TAMISEMI, OMR, MoH, Halmashauri zote |
| Kuandaa na kutekeleza kampeni za uelimishaji kuhusu mbinu za usimamizi wa taka | Halmashauri zote | Mipango ya kampeni ya uelimishaji kwa uma kuandaliwa na kusambazwa | Idadi ya nyaraka zilizoandaliwa na kusambazwa | Nyaraka zilizoandaliwa | 2025-2030 | 0.368 | OR-TAMISEMI, OMR, MoH, Halmashauri |
| Kukuza uelewa kwa wakusanya taka kuhusu utenganishaji wa taka majumbani na katika maeneo ya biashara | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | 50% ya wakusanya taka kushiriki katika programu | Idadi ya wakusanya taka | Ripoti | 2025-2030 | 1.5 | OR-TAMISEMI, OMR MoH, NEMC, majiji ya Dar es |

| Shughuli | Maeneo ya Kipaumbele | Shabaha | Kiashiria | Njia za uthibitishaji | Muda wa utekelezaji | Makadirio ya bajeti (TShs 'Bilioni) | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | Salaam, Dodoma, Arusha, Mbeya, Mwanza, Tanga |
| Kufanya kampeni za uelimishaji kuhusu njia za kupunguza taka kwa taasisi (shule, magereza, kambi za kijeshi) na viwanda. | Mamlaka zote za Serikali za Mitaa | Elimu ya uelewa wa mbinu za kupunguza taka kufanyika katika majiji 6 | Idadi ya shule, magereza, kambi za kijeshi na viwanda. | Ripoti | 2025-2030 | 1.5 | OR-TAMISEMI, OMR MoH, NEMC, majiji ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mbeya, Mwanza, Tanga |
| Kutoa mafunzo kwa wafanya uamuzi (viongozi wa serikali, wanasiasa) kuhusu utekelezaji wa sheria ndogo na sheria za mazingira zinazohusu usimamizi wa taka. | Majiji na Manispaa | Majiji 6 na manispaa 20 | Idadi ya wafanya uamuzi waliopatiwa mafunzo | Ripoti | 2025-2030 | 1 | OR-TAMISEMI, OMR, MoH, majiji na manispaa zote |
| Kuandaa video na nyaraka za mafunzo kwa ajili ya ziara ya kwa shule za msingi. | Halmashauri zote | 20% ya shule za msingi kujumuishwa katika program ya ziara | Idadi ya shule za msingi zilizojumuishwa katika program ya ziara | Ripoti | 2025-2030 | 0.2 | OR-TAMISEMI, OMR, MoH, NEMC, Mamlaka zote za Serikali za |

| Shughuli | Maeneo ya Kipaumbele | Shabaha | Kiashiria | Njia za uthibitishaji | Muda wa utekelezaji | Makadirio ya bajeti (TShs 'Bilioni) | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | Mitaa |
| **Jumla Ndogo** | | | | | | **7.768** | |
| **JUMLA KUU** | | | | | | **434.698** | |

## 5.2 Mahitaji na Upatikanaji wa Rasilimali Fedha

Utekelezaji wa Mkakati huu unakadiriwa kugharimu Shilingi za Kitanzania 434,498,000,000 katika kipindi cha miaka 5 (2025 - 2030) ya utekelezaji wake. Vyanzo vya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati ni pamoja bajeti ya Serikali, wadau wa maendeleo, sekta binafsi na asasi za kiraia

## 5.3 Utaratibu wa Utekelezaji

Utekelezaji wa Mkakati huu unahitaji ushiriki madhubuti wa wadau wakuu. Mkakati huu umebainisha na kugawa majukumu na wajibu kwa taasisi mbalimbali za Serikali na wadau wasio wa serikali kama ilivyoainishwa hapa chini.

Utekelezaji wa Mkakati huu utazingatia utaratibu wa kitaasisi ulioainishwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191. Hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais (OMR), itaratibu utekelezaji wa Mkakati huu, kwa kushirikiana na Wizara zenye dhamana ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Afya. Aidha, OMR itaunda Kikosikazi cha wataalamu wa kusimamia utekelezaji wa Mkakati. Kikosikazi cha wataalamu kitakuwa na jukumu la kushauri masuala ya utekelezaji wa Mkakati na usimamizi wa taka nchini. Kikosikazi kitajumuisha Wizara zenye dhamana ya mazingira, Mamlaka za Serikali ya Mitaa, Afya; Maji, Viwanda, Biashara na Uwekezaji, na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

### 5.3.1 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa na jukumu la kudhibiti taka katika maeneo yao, hasa kudhibiti na kupunguza uzalishaji wa taka kwenye vyanzo. Pia, zitatunga sheria ndogo ili kuimarisha utoaji wa huduma za usimamizi wa taka kwa kufanya tafiti za mara kwa mara za kuainisha kiasi na aina ya taka zinazozalishwa. Pamoja na majukumu hayo, Mamlaka zina wajibu pia wa kusimamia ukusanyaji wa taka katika maeneo ya mijini na pembezoni mwa miji na kuanzisha vituo vya utenganishaji wa taka na kuwezesha upatikaji wa makasha ya kuhifadhi taka. Vilevile, Mamlaka zina jukumu la kuhakikisha kuwa viwanda vyote vinasimamia na kudhibiti taka zinazozalishwa.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaainisha changamoto, na kuweka kipaumbele cha ugawaji wa rasilimali za kutekeleza afua zilizopangwa katika usimamizi wa taka. Aidha, halmashauri zitapaswa kutenga na kuweka mipaka ya maeneo ya kutosha kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa taka.

### 5.3.2 Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Majukumu ya Wizara hii ni kuratibu na kusimamia maendeleo ya mikoa, hivyo kuratibu sera na mikakati ya usimamizi wa maendeleo ya miji pamoja na shughuli za Sekretarieti za Mikoa. Aidha, Wizara itakuwa na jukumu la kuwezesha utekelezaji wa Mkakati huu kwa kutoa miongozo ya kimkakati na kujenga uwezo, ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa rasilimali watu na fedha katika kutekeleza shughuli za usimamizi wa taka.

### 5.3.3 Wizara yenye dhamana ya Mazingira

Wizara yenye dhamana ya Mazingira itakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia kwa ujumla utekelezaji wa mkakati huu, ufuatiliaji na tathmini kwa kushirikiana na wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuhamasisha ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mkakati.

### 5.3.4 Wizara yenye dhamana ya Afya

Wizara ya Afya ina wajibu wa kutunga sera, sheria, miongozo inayohusiana na afya; uhamasishaji wa utafutaji wa rasilimali fedha; na uratibu wa shughuli za sekta ya afya. Wizara itahakikisha kunakuwa na usimamizi endelevu wa taka, ikijumuisha uhifadhi wa taka kwa muda, usafirishaji na utupaji salama wa taka. Wizara ya Afya pia itakuwa na jukumu la kusajili watoa huduma za afya na usimamizi wa taka chini ya Sheria ya Wahudumu wa Afya ya Mazingira (Usajili) ya mwaka 2007.

### 5.3.5 Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

Baraza lina jukumu la kutekeleza na kuhakikisha uzingatiaji wa sheria za usimamizi wa mazingira; kufanya mapitio, ukaguzi na ufuatiliaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii; kuimarisha mawasiliano ya masuala ya mazingira, elimu, uelewa wa umma; na utafiti kuhusu usimamizi bora wa mazingira kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali ya Mitaa. Katika kutekeleza Mkakati huu, Baraza litahakikisha usimamizi wa taka unaozingatia hifadhi ya mazingira; kufanya utafiti; kuwezesha mafunzo; kukuza uelewa kwa lengo la kufikia jamii kuhusu usimamizi endelevu wa taka.

### 5.3.6 Wizara za Kisekta

Wizara za Kisekta zitakuwa na jukumu la kusaidia utekelezaji wa Mkakati huu ili kuimarisha usimamizi bora wa taka. Wizara za kisekta zitawajibika kuhakikisha kuwa masuala ya usimamizi wa taka yanajumuishwa katika sera, mikakati, mipango, programu na miradi ya sekta husika

### 5.3.7 Idara na Wakala wa Serikali

Idara na Wakala wa Serikali zitatekeleza Mkakati huu katika Mamlaka zao kwa kujumuisha afua za usimamizi wa taka katika mikakati, programu na mipango yao ya maendeleo

### 5.3.8 Asasi za Kiraia

Asasi za kiraia zina mchango mkubwa kwa Serikali katika kuhamasisha jamii na kutafuta rasilimali fedha katika shughuli za usimamizi wa taka. Asasi za Kiraia za kitaifa na kimataifa zitashiriki katika utekelezaji wa mkakati huu, katika kukuza uelewa wa jamii kuhusu usimamizi wa taka, kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha za kusaidia utekelezaji wa afua zilizoainishwa katika mkakati huu.

### 5.3.9 Sekta Binafsi

Sekta binafsi zitakuwa na jukumu la kutafuta na kuwekeza katika fursa mbalimbali zinazohusiana na usimamizi wa taka ili kuwezesha utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa taka, kukuza na kuhawilisha teknolojia sahihi za usimamizi wa taka, na kukuza uelewa kwa umma.

### 5.3.10 Taasisi za Elimu na Utafiti

Taasisi za elimu na tafiti zitahusika na utafiti, mafunzo, ukuzaji wa teknolojia, kukuza uelewa na kusambaza matokeo ya utafiti katika shughuli za usimamizi wa taka.

### 5.3.11 Wadau wa Maendeleo

Washirika wa Maendeleo watawezesha utekelezaji wa mkakati huu kwa kutoa rasilimali fedha na ufundi, kuhawilisha teknolojia na kujenga uwezo, miongoni mwa wadau.

### 5.3.12 Wanajamii

Wanajamii (kata, mtaa) watatekeleza mkakati huu katika shughuli zao za kila siku kwenye maeneo yao ya kijiografia. Hii itahusisha ushiriki wao katika shughuli za usimamizi wa taka.

### 5.3.13 Vyombo vya Habari

Jukumu la vyombo vya habari litakuwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati za usimamizi wa taka kwa umma. Jukumu hili litafanyika kwa ushirikiano na wizara yenye dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine kuandaa kampeni za elimu ya usimamizi wa taka.

# SURA YA SITA: UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI

## 6.1 Mpango wa Ufuatiliaji, Mapitio na Tathmini

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Udhibiti wa Taka (2025-2030) utazingatia Mwongozo wa tathmini na ufuatiliaji. Aidha, program za ufuatiliaji na tathmini zitajikita katika, malengo na matokeo ili kutathmini hali ya utekelezaji na kupendekeza hatua stahiki zinazotakiwa kuchukuliwa. Hatua hii itahitaji rasilimali, zana stahiki za ufuatiliaji, uchambuzi wa takwimu, mifumo madhubuti ya utoaji wa taarifa na ushirikishwaji wa wadau. Ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa ni nyenzo muhimu zitakazotumika na wizara zinazohusika na Serikali za Mitaa, Mazingira, Afya na Maji ambazo ni wadau wakuu katika usimamizi wa taka kwa ajili ya kufanya uamuzi wa pamoja na kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka wa 2025–2030.

### 6.1.1 Umuhimu wa ufuatiliaji

Ufuatiliaji wa mkakati unalenga kuhakikisha rasilimali zilizotengwa kutekeleza Mkakati zinatumika kulingana na bajeti iliyopitishwa, muda uliopangwa pamoja na kuhakikisha matokeo yanayotarajiwa yanapatikana kwa wakati na kwa gharama halisi. Vilevile, ufuatiliaji utawezesha upatikanaji wa taarifa kwa Wizara yenye dhamana ya mazingira na wadau mbalimbali kuhusu usimamizi endelevu wa taka kulingana na matumizi ya fedha zilizotengwa.

### 6.1.2 Umuhimu wa tathmini

Kazi ya tathmini itahusisha uchambuzi wa kina wa ufanisi na athari za matokeo ya utekelezaji wa Mkakati kulingana na malengo yaliyotarajiwa. Aidha, tathmini hii itawawezesha watoa maamuzi kutoa maelekezo stahiki ya kuboresha utekelezaji wa Mkakati. Katika kipindi cha miaka mitano (5) ya utekelezaji wa Mkakati tathmini zitafanywa mara mbili, ambapo tathmini ya kati itafanyika mwaka 2027 na tathmini ya mwisho itafanyika mwaka 2030.

### 6.1.3 Tathmini ya Utekelezaji wa Mkakati

Tathmini ya utekelezaji wa Mkakati itaratibiwa na OMR kwa kushirikiana na Wizara zenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Afya na Mazingira. Aidha, kikosikazi cha wataalamu cha usimamizi wa taka kitaanzishwa kikiwa na jukumu la kupanga, kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali fedha, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini mikakati ya usimamizi wa taka. Kikosikazi kitaitisha mikutano ya mapitio kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali 4 hapa chini;

**Jedwali 4: Ratiba ya utekelezaji wa Mkakati**

| Na. | Aina ya mikutano | Muda | Viongozi | Wahusika |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mikutano ya robo mwaka | Kila robo mwaka | Katibu Mkuu (OMR) – Mwenyekiti<br><br>Katibu Mkuu (OR –TAMISEMI) – Mwenyekiti Mwenza<br><br>Katibu Mkuu Wizara ya Afya – Mwenyekiti Mwenza<br><br>Katibu Mkuu Wizara ya Maji – Mwenyekiti Mwenza | Wakuu wote wa Idara, vitengo, na sehemu kutoka OMR, OR-TAMISEMI, NEMC, Bodi za mabonde ya maji na Mamlaka za maji |
| 2. | Mikutano ya mwaka | Mwisho wa mwaka | Katibu Mkuu (OMR) – Mwenyekiti<br><br>Katibu Mkuu (OR-TAMISEMI – Mwenyekiti Mwenza<br><br>Katibu Mkuu Wizara ya Afya – Mwenyekiti Mwenza<br><br>Katibu Mkuu Wizara ya Maji – Mwenyekiti Mwenza | Wakuu wote wa Idara, vitengo, na sehemu kutoka OMR, OR-TAMISEMI, NEMC, Bodi za mabonde ya maji na Mamlaka za maji |

## 6.2 Mpango wa utoaji wa Taarifa za Usimamizi wa Taka

Mpango huu utahusisha utoaji wa taarifa wa hatua iliyofikiwa katika kufikia malengo ikilinganishwa na matumizi ya fedha. Mpango wa Utoaji Taarifa utaainisha kwa kina utoaji taarifa za ndani na za nje.

### 6.2.1 Mpango wa Utoaji Taarifa Ndani

Utoaji wa taarifa wa utekelezaji wa Mkakati utafanywa na Wizara zenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; mazingira, afya; na maji ambazo ni wadau wakuu wa usimamizi wa taka na itahusisha uandaaji wa taarifa za fedha na utekelezaji; taarifa za mwaka, taarifa za nusu mwaka pamoja na matokeo yaliyopatikana. Taarifa zitajumuisha aina ya taarifa, wapokeaji, muda wa taarifa na taasisi zinazohusika. Taarifa hizi zitawasilishwa kwa wadau wa nje kama vile Wizara, Bunge na Umma. **Jedwali 5** hapa chini linafafanua zaidi mpango wa utoaji taarifa

**Jedwali 5: Mpango wa Ndani wa utoaji taarifa**

| Na. | Aina ya Taarifa | Mpokea Taarifa | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Taarifa ya utekelezaji ya kituo | Mkuu wa Idara au Kitengo | Kila wiki | Mkurugenzi Msaidizi na maofisa |
| 2. | Taarifa ya utekelezaji wa mkakati | Katibu Mkuu | Kila robo mwaka | Mkurugenzi na Wakuu wa Vitengo |
| 3. | Taarifa ya utekelezaji ya robo mwaka | Katibu Mkuu | Kila robo mwaka | Mkurugenzi na Wakuu wa Vitengo |
| 4. | Taarifa ya utekelezaji ya mwaka | Katibu Mkuu | Kila mwaka | Mkurugenzi na Wakuu wa Vitengo |

### 6.2.2 Mpango wa Utoaji Taarifa Nje

Utoaji wa taarifa nje za utekelezaji wa Mkakati utafanywa na Wizara zenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; mazingira, afya; na maji ambazo ni wadau wakuu wa usimamizi wa taka na itahusisha uandaaji wa taarifa za fedha na utekelezaji; taarifa za mwaka, taarifa za nusu mwaka pamoja na matokeo yaliyopatikana. Taarifa zitajumuisha aina ya taarifa, wapokeaji, muda wa taarifa na taasisi zinazohusika. Taarifa hizi zitawasilishwa kwa wadau wa nje kama vile Wizara, Bunge na Umma. **Jedwali 6** hapa chini linafafanua zaidi mpango wa utoaji taarifa.

**Jedwali 6: Mpango wa utoaji taarifa nje**

| Na. | Aina za Taarifa | Mpokeaji wa Taarifa | Muda | Mhusika | Na. |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | Robo mwaka | OR-TAMISEMI, OMR, Wizara ya Afya na Wizara ya Maji | Robo mwaka | • Katibu Mkuu (OMR)-Mwenyekiti<br>• Katibu Mkuu (OR-TAMISEMI_-Mwenyekiti Mwenza<br>• Katibu Mkuu (Wizara ya Afya) - Mwenyekiti Mwenza<br>• Katibu Mkuu |
| 2. | | Taarifa ya tathmini ya mwisho | TAMISEMI OMR, Wizara ya Afya, Wizara ya Maji | Mara moja | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | (Wizara ya Maji) - Mwenyekiti Mwenza |

### 6.3 Utaratibu wa Ufuatiliaji wa Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Taka

Mfumo huu utajumuisha takwimu za ufuatiliaji zitakazochukuliwa kwenye Mkakati zinazojumuisha ufuatiliaji wa takwimu za usimamizi wa taka kutoka Wizara za kisekta. Uwasilishaji wa taarifa kwa ajili ya ufuatiliaji utazingatia matumizi ya mfumo wa kielektroniki. Mfumo huu utawezesha upatikanaji wa takwimu kwa wakati na kuongeza kasi ya uwasilishaji wa taarifa.

**Jedwali 7: Matokeo ya utekelezaji wa Mkakati**

| Lengo la kimkakati | Na. | Shughuli | Viashiria | Matokeo ya muda wa kati | Matokeo ya muda mrefu |
|---|---|---|---|---|---|
| **1. Kuhamasisha Upunguzaji wa Taka kupitia dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza** | 1.1 | Kuimarisha utenganishaji wa taka katika ngazi ya kaya | Idadi ya nyumba zinazofanya utenganishaji wa taka | • Kiwango cha utenganishaji taka kuongezeka<br>• Kutenga taka<br>• Kupunguza kiwangio cha taka<br>• Urejelezaji taka kuongezeka<br>• Taka kurejelezwa na kuzalisha nishati<br>• Kukuza ushiriki wa sekta binafsi | Taka kupungua katika madampo |
| | 1.2 | Kuimarisha uchambuzi wa taka katika vituo vya kukusanyia taka | Idadi ya vituo vya uchambuzi vilivyofanyiwa majaribio | | |
| | 1.3 | Kufanya kampeni za kuelimisha umma kuhusu utenganishaji na uchambuzi wa taka | Idadi ya kempeni za umma zilizofanyika | | |
| | 1.4 | Kutoa mwongozo wa kitaalamu na utenganishaji wa taka kwa kuzingatia rangi | Asilimia ya watu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotumia rangi kutenga taka | | |
| | 1.5 | Kuanzisha au kuimarisha vituo vya kutenganisha taka | Idadi ya vituo vya kutengajisha taka viilivyoanzishwa | | |
| | 1.6 | Kuanzisha au Kuimarisha vituo vya uchakataji wa awali wa taka | Idadi ya vituo vya uchakataji wa awali wa taka vilivyoanzishwa | | |
| | 1.7 | Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi | Idadi ya mikataba | | |

| Lengo la kimkakati | Na. | Shughuli | Viashiria | Matokeo ya muda wa kati | Matokeo ya muda mrefu |
|---|---|---|---|---|---|
| | | katika urejelezaji taka | rasmi na sekta binafsi | | |
| | 1.8 | Kuanzisha au kuimarisha vituo vya uzalishaji wa mboji | Idadi ya vituo vya kutengeneza mboji vilivyoanzishwa | | |
| | 1.9 | Kuanzisha vituo vya kuzalisha nishati kwa kutumia taka | Idadi ya vituo vya kuzalisha nishati kwa kutumia taka | | |
| | 1.10 | Kuanzisha au kuimarisha vituo vya mwisho vya utupaji taka | Idadi ya madampo yaliyoanzishwa au kuboreshwa | | |
| **2. Kuinarisha Ushughulikia wa Taka** | 2.1 | Kuimarisha ushirikiano na wadau katika miradi ya usimamizi wa taka | Idadi ya wadau walioshirikishwa | Kuwapo kwa miundombinu madhubuti ya ukusanyaji, usafirishaji, vituo vya uchakataji na utupaji wa taka inayozingatia usalama wa mazingira. | |
| **3. Kuimarisha usimamizi endelevu wa majitaka** | 3.1 | Kutenga na kuweka mipaka katika maeneo ya vituo vya usimamizi wa taka | Idadi ya Hekta zilizotengwa na kuwekewa mipaka | • Taka chache kutupwa bila kuchakatwa | Mazingira kuwa safi |
| | 3.2 | Kuanzisha na kuimarisha mitambo na | Idadi ya mitambo | | |

| Lengo la kimkakati | Na. | Shughuli | Viashiria | Matokeo ya muda wa kati | Matokeo ya muda mrefu |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mabwawa ya kutibu majitaka | na mabwawa ya kuchakata majitaka | • Kuwapo kwa vituo vya kuchakata taka | |
| | 3.3 | Kuimarisha na kutumia teknolojia madhubuti za kuchakata majitaka na takakinyesi | Idadi ya mitambo ya kutibu majitaka | | |
| | 3.4 | Kuimarisha utekelezaji wa program za utumiaji tena wa majitaka yaliyorejelezwa kwa angalau 50% ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | Idadi ya program | | |
| | 3.5 | Kuimarisha utumiaji wa DEWATS | Idadi ya DEWATS | | |
| | 3.6 | Kumarisha usimamizi wa maji ya mvua | Idadi ya kaya na taasisi zinazotumia teknolojia ya usimamizi wa maji ya mvua | | |
| | 3.8 | Kuimarisha usafi katika miundombinu ya maji ya mvua | Idadi ya mipango | | |
| **4. Kuimarisha Uwezo wa Kitaasisi katika udhibiti na** | 4.1 | Kuimarisha mfumo wa ugharimiaji wa usimamizi wa taka | Idadi ya halmashauri | Kupunguza kiwango cha taka | Kukuza uwezo wa kitaasisi katika usimamizi wa taka |
| | 4.2 | Kuimarisha utekelezaji wa nyenzo za usimamizi wa taka | Idadi ya mipango, miongozo na sheria | | |

| Lengo la kimkakati | Na. | Shughuli | Viashiria | Matokeo ya muda wa kati | Matokeo ya muda mrefu |
|---|---|---|---|---|---|
| **usimamizi wa Taka.** | | | ndogo zilizoandaliwa | | |
| | 4.3 | Kushirikisha sekta isiyo rasmi katika usimamizi wa taka | Idadi sekta zisizo rasmi zilizorasimishwa | | |
| | 4.4 | Kuimarisha utafiti na kusambaza teknolojia bunifu | Idadi ya sheria ndogo zilizopitiwa na kurekebishwa | | |
| | 4.5 | Kuimarisha usimamizi wa taka katika ngazi ya kata, kijiji na mtaa | Idadi ya wafanyakazi walioajiriwa au kuteuliwa | | |
| | 4.6 | Kuanzisha mfumo wa taarifa za usimamizi wa taka. | Idadi ya mifumo ya taarifa iliyoanzishwa | | |
| | 4.7 | Kuimarisha ufuatiliaji na hatua za utekelezaji wa sheria ili kushughulikia ukiukwaji wa mifumo ya usimamizi wa taka. | Asilimia ya uzingatiwaji wa sheria | | |
| | 4.8 | Kufanya ufatiliaji na tathmini ya mkakati | Idadi ya shughuli zilizotekelezwa | | |
| **5.** Kukuza Uelewa wa Umma, Ushirikishwaji wa Jamii na sekta binafsi | 5.1 | Kuandaa na kutekeleza mpango wa kukuza uelewa kuhusu mbinu za usimamizi wa taka | Idadi ya mipango iliyoandaliwa | Mwenendo wa jamii kuhusiana na usimamizi wa taka kubadilika | Kupungua kwa magonjwa na vifo |
| | 5.2 | Kuanda nyaraka kuhusiana na usimamizi wa taka | Idadi ya nyaraka zilizoandaliwa na kusambazwa | | |

| Lengo la kimkakati | Na. | Shughuli | Viashiria | Matokeo ya muda wa kati | Matokeo ya muda mrefu |
|---|---|---|---|---|---|
| | 5.3 | Kufanya kampeni za uhamasishaji kwa wakusanyaji wa taka ili kuhimiza utenganishaji wa taka katia chanzo katika ngazi ya kaya na biashara. | Idadi ya wakusanya taka | | |
| | 5.4 | Kufanya kampeni za uhamasishaji kuhusu mbinu za kupunguza uzalishaji wa taka kwa taasisi kama shule, magereza, kambi za jeshi, na viwanda. | Idadi ya taasisi mbalimbali kama shule, magereza, kambi za jeshi, na viwanda | | |
| | 5.5 | Kufanya mafunzo kwa wafanya uamuzi (viongozi wa serikali, wanasiasa) kuhusu utekelezaji wa sheria ndogo na sheria za mazingira zinazohusiana na usimamizi wa taka | Idadi ya wafanya uamuzi waliopewa mafunzo | | |
| | 5.6 | Kukuza ushiriki wa jamii katika siku ya usafi Kitaifa | Idadi ya halmashauri | | |
| | 5.7 | Kufanya mashindano ya mwaka ya afya na mazingira | Idadi ya halmashauri zilizoshiriki mashindano | | |
| | 5.8 | Kutengeneza video na vifaa vya elimu kwa ajili ya ziara ya uhamasishaji katika shule za msingi. | Idadi ya shule za msingi zilizojumuishwa katika ziara ya uhamasishaji | | |

**Jedwali 8: Orodha ya wataalam walioandaa Mkakati**

| Na. | Jina | Taasisi | Wadhifa |
|---|---|---|---|
| 1. | Bi. Kemilembe Mutasa | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 2. | Bw. Thomas Chali | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 3. | *Mha*. Onesphory Kamukuru. | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 4. | *Mha*. Joseph Kiruki | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 5. | Dkt. Makuru J. Nyarobi | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 6. | Bw. Richard Masesa | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 7. | Bw. Shadrack S. Nyanda | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 8. | *Mha*. Julius Enock | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 9. | Bi. Jeniva Olengeile | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 10. | Bi. Getrude Sombe | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 11. | Bi. Annamaria Gerome | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 12. | Bw. Said Athuman | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 13. | *Mha*. Abdulahmid Makame | Ofisi ya Makamu wa Rais | Mjumbe |
| 14. | Bw. Theodory Mulokozi | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) | Mjumbe |
| 15. | Bw. Evance Simkoko | Wizara ya Afya | Mjumbe |
| 16. | *Dkt*. Befrina Igulu | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) | Mjumbe |
| 17. | *Mha*. Fredrick Ligate | Chuo Kikuu Ardhi (ARU) | Mjumbe |
| 18. | *Mha*. Edwin Ndibalema | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) | Mjumbe |
| 19. | Bw. Ally Mfinanga | Halmashauri ya Jiji la Dodoma | Mjumbe |
| 20. | Bw. Kizito Nkwabi | Halmashauri ya Jiji la Tanga | Mjumbe |
| 21. | Dkt. Fatuma Mlaki | Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) | Mjumbe |
| 22. | *Mha*. Rose Edward | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) | Mjumbe |